# Pambazuko

Toleo Namba 141 | Jumatatu, Septemba 29-Oktoba 5,2025




*Wanafunzi kutoka Shule ya ProCivitas Helsingborg ya nchini Sweden ambao ni marafiki wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Barbro Johansson, wakionyesha umahiri wa kucheza ngoma ya Kimasai wakati wa mahafali ya Kidato cha Nne na maadhimisho ya miaka 25 ya kuanzishwa kwake, Dar es Salaam jana. (Picha na Fidelis Felix).*

# Utafiti: Rais Samia anaaminika zaidi

Uk. 6&7



**"Sisi tuliamua kufanya utafiti huu kwa hiari kwa kila aliyefikiwa, wapo baadhi waligoma, hawakupenda kutoa maoni yao, na wapo waliojibu maswali kadhaa na wengine kuacha baadhi,"alisema Rwemugize.**

# Vyama vya upinzani 'vyakata pumzi'

Uk. 9&11

- Havina fedha kuendesha kampeni

**Biashara**

## Ripoti: Tanzania yakua haraka kibiashara Afrika

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazokua kwa kasi kwenye uchumi – unaochochewa na biashara, kwa nchi za Afrika. Hali hiyo inatokana na kuwepo mazingira mazuri ya kufanya biashara – kati ya Tanzania na mataifa mengine....

Habari Uk. 18

Tahariri/Katuni

# Tuepuke tamaa ya vurugu, tulinde amani

KUNA baadhi ya Watanzania wameanza kuingiwa hofu kutokana na matamshi yanayotolewa na baadhi ya watu kuhusu kuwepo kwa maandamano ya "kuikataa serikali iliyopo."

Matamshi hayo yanatolewa na baadhi ya watu, hasa walioko mitandaoni, ambapo wanahimiza Oktoba 29, mwaka huu, watu wajitokeze kuingia barabarani kuandamana ili kuonyesha namna wasivyopenda baadhi ya mambo yanayofanyika nchini Tanzania.

Tayari Jeshi la Polisi imeonya wanaoendelea kuhamasisha maandamano hayo kuacha mara moja na kwamba wanaofanya hivyo, wanatenda uhaini, ambalo ni kosa la jinai.

Sambamba na msimamo wa jeshi hilo, Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akitumia mikutano ya kampeni zake kuwaeleza wananchi kuwa wasiwe na hofu kwamba maandamano hayo yatafanyika na kuleta taharuki, kwa kuwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama vimejipanga kuhakikisha amani inatawala sasa na hata siku inayotangazwa kuwepo kwa maandamano hayo.

Maandamano yanayohimizwa yanatangazwa kufanyika Oktoba 29, siku ambayo ndiyo itatumika kwa Watanzania kwenda kwenye vituo vya kupiga kura kuchagua viongozi wao kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kutokana na kauli na msimamo huo wa Polisi na Rais Samia, bado mabingwa wa mitandao wakisisitiza kuendelea kuhamasisha watu waandamane siku hiyo, huenda kuna hofu imejengeka kwa Watanzania.

Sisi Pambazuko tunapenda kusisitiza kuwa tunaamini kuwa maandamano ni suala ambalo linaruhusiwa kisheria, lakini linapopangwa kufanyika kwa kukaidi, huenda kukatokea rabsha na hasara kubwa kwani vyombo vya ulinzi na usalama havitakuwa tayari kuona hali ya utulivu inavunjwa, tena siku ambayo kuna haki nyingine – ya kupiga kura inaenda kutekelezwa.

Ni ukweli usiopingika kuwa upigaji kura ni moja ya matukio muhimu katika mchakato wa demokrasia nchini. Siku hii aghalabu huja mara chache sana na kwa uchaguzi mkuu ni siku moja kila baada ya miaka mitano.

Hivyo, kupanga kuivuruga siku hii kwa namna yoyote, ni jambo lisilokubalika ingawa hatumaanishi kuwa wanaopanga kuandamana wamepanga kufanya vurugu kwani maandamano yanaweza kufanyika bila kuwepo kwa vurugu.

Kwa kuwa zipo siku nyingine nyingi ambazo watu wanaweza kuandamana, ni rai yetu kuwa maandamano haya yangepangiwa siku nyingine ili kutoa fursa kwa tukio hili kubwa kufanyika bila bughudha.

Endapo kutatokea wenye vichwa ngumu kuendelea kukaidi amri zinazotolewa na mamlaka na kuamua kuingia barabarani, siyo kwenda kupiga kura, bali kuandamana, kunaweza kutokea yasiyotarajiwa na hivyo kuharibu taswira ya amani ya Tanzania, jambo ambalo Pambazuko haipendi litokee.

## Katuni



# Miundombinu...



Majitaka yakiwa yametuama katika Barabara ya Lumumba yaliyosababishwa na ubovu wa miundombinu kuziba kutokana na ujenzi usiofuata taratibu maeneo ya Kariakoo, Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu).

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

## WASILIANA NA CHUMBA CHA HABARI; 0784 211 716

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na pale

## Shelisheli kurudia uchaguzi

SHELISHELI imepanga kurejewa kwa uchaguzi mkuu wa nchi hiyo, baada ya kukosekana mshindi wa kiti cha urais. Sasa kura zitapigwa kwenye mchuano wa wagombea wawili wa nafasi hiyo. Tarehe ya marudio ya uchaguzi bado haijatangazwa.

Katika uchaguzi uliofanyika mwishoni mwa wiki, mpinzani Patrick Herminie alipata asilimia 48.8 ya kura, wakati mgombea, Wavel Ramkalawan, alipata asilimia 46.4, kulingana na matokeo rasmi. Mgombea anahitaji kushinda zaidi ya asilimia 50 ya kura ili kutangazwa mshindi.

Herminie anawakilisha chama cha United Seychelles, ambacho kilitawala siasa kwa miongo kadhaa nchini humo kabla ya kupoteza madaraka miaka mitano iliyopita. Ramkalawan anasaka muhula wa pili kama kiongozi wa nchi hiyo ndogo zaidi Afrika.



## Ufaransa yakaliwa kooni

WAZIRI Mkuu wa Serikali ya Mpito ya Niger, Lamine Zeine Ali Mahaman (pichani), amekosoa Ufaransa, ambayo ni mkoloni wa zamani wa nchi hiyo, akisema kuwa taifa hilo la Ulaya linatumia "ugaidi" kudhoofisha nchi yake.

Amesema kuwa tangu wanajeshi wa Ufaransa walipotimuliwa kutoka Niger mwaka 2023, serikali ya nchi hiyo imeanzisha mpango wa siri wa kuhujumu nchi yake.

Mahaman anadai kuwa Ufaransa imekuwa ikifadhili na kufundisha magaidi ili kuvuruga amani na maendeleo ya nchi hiyo. Pia anadai Ufaransa inachochea vita vya kikabila.

## Palestina yatetewa Afrika

ZAIDI ya watu 3,000 waliandamana barabarani kwenye Jiji la Cape Town, Afrika Kusini juzi – Jumamosi wakishinikiza nchi yao kuvunja uhusiano wa kidiplomasia na kibiashara na Israel, ili kuonyesha kuchukizwa na uvamizi wa nchi hiyo ndani ya ardhi ya Palestina, hasa vita vya Gaza.

Afrika Kusini imekuwa mkosoaji mkubwa wa uamuzi wa Israel kushambulia Gaza na kusababisha mauaji ya watu wengi wasiokuwa na hatia, hasa wanawake na watoto. Afrika Kusini iliishitaki Israel Mahakama Kuu ya Umoja wa Mataifa Desemba 2023.

Maandamano ya Jumamosi yalikusanya pamoja mashirika kadhaa yanayounga mkono Palestina, vyama vya kisiasa, na makundi ya Waislamu na Wakristo, katika moja ya mikusanyiko mikubwa zaidi ya aina hiyo kwa miezi kadhaa.

## M23 hawataki kupoa DRC

PAMOJA na "kelele za dunia" kutaka kundi la waasi la M23 linaloendelea kukwamisha amani na usalama wa maeneo kadhaa ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kuacha mapigano, bado linaweka pamba masikioni. Halitaki kusitisha vita.

Taarifa zinaeleza kuwa kundi hilo la M23, linalodaiwa kupewa ufadhili wa fedha na Serikali ya Rwanda, limezidisha mauaji katika maeneo jirani na Goma! Rwanda imekuwa ikikataa kuhusika kwa lolote na M23.

Umoja wa Mataifa umekuwa ukisisitiza kusitishwa kwa mapigano kati yake na majeshi ya DRC, kwa ajili ya kulinda usalama na kuweka mazingira ya usalama kwa wananchi wote. Hadi sasa M23 linatamba kushikilia miji kadhaa ikiwamo Goma.



Na Mzee TAI

# Sijui tukoje, hata Simbu tumemtosa, kha!

NIMEAMKA asubuhi leo nikiwa bado na majonzi ya kumpoteza rafiki, ndugu na mshauri wangu wa maisha; Baba+ Askofu Dkt. Stephen Ismail Munga.

Askofu Munga alifariki Jumamosi iliyopita akiwa anaendelea kupata matibabu hospitalini jijini Dar es Salaam, hakika ni kilio na kumbukumbu isiyoweza kufutika kwenye kichwa changu. Kimekuwa kifo cha ghafla sana. Alale salama Askofu Munga.

Wakati nikiendelea kumlilia Askofu Munga, mara nakutana na picha kwenye dirisha la mtandao wangu wa WhatsApp.

Hapo namuona mwanariadha Alphonce Simbu akiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), akiwa amebeba shada kubwa la maua.

Niliposoma zaidi nakutana na maelezo kwamba ndiyo alikuwa akiwasili kutoka Tokyo, Japan, ambako aliibuka kidedea kwa kuwa bingwa wa dunia kwa mbio ndefu za Marathon – Kilomita 42, mwaka huu.

Kwanza nilishtuka, iweje Simbu anawasili kimyakimya bila Watanzania wengi kujua. Kwanini anakuja kama kimyakimya vile? Nani amepanga safari ya kuwasili usiku wa manane?

Nikavuta miwani yangu ili kutazama vyema kuwatambua "wakubwa" waliokwenda kumpokea mwana huyu wa Tanzania aliyetutoa kimasomaso kwa kupata dhahabu.

Nikatazama zaidi, sikuona mkubwa sana hata mmoja, na wakati naendelea "kung'ang'aza macho, nakutana na kamanda mmoja, mwanadada akiwa amevalia mavazi rasmi ya jeshi letu la wananchi, JWTZ. Pia nikaona wamama kadhaa, baadaye naambiwa mmoja wao ni mama yake mzazi shujaa wetu Simbu.

Nikabaki nimebung'aa! Kwamba wako wapi vigogo? Yuko wapi Kassim Majaliwa, yule waziri wetu mkuu, nikamuwaza Palamagamba Kabudi, huyuuu waziri wetu wa michezo, wakanijia kichwani viongozi kadhaa ambao nilidhani lazima wangekuwepo kumpokea Simbu.

Nikawaza kuhusu mkuu wa majeshi yetu, huyu anaitwaa Jenerali Jacob John Mkunda, nikanyanyua simu kumpigia, nikasita. Nikamuacha.



*Mwanariadha Alphonce Simbu*

Nikajiuliza zaidi; hivi hawa wakubwa walikuwa wapi. Je, wamelala kweli na kuiacha heshima ya Tanzania ishuke kimyakimya bila uwepo wao? Wana raha gani kwani?

Baadaye nikafikiria kitu. Iweje watu wetu wa itifaki nao waruhusu Simbu awasili usiku wa manane? Walishindwa nini kupanga ndege nyingine awasili mapema ili watu wengi wajitokeze barabarani kumlaki mwana huyu wa Tanzania?

Hata kama tiketi yake ilikuwa inakatwa na waandazi, kwanini tusingeiacha na kukata nyingine ya kuwasili mapema wakati jua halijazama? Sijui sisi tukoje, yaani mambo muhimu tunayaweka kapuni na kuyapa uzito mwepesi!

Hata hivyo, pamoja na mazonge haya ya wakubwa wetu, siku iliyofuata nikamuona Jenerali Mkunda amefanya jambo zuri. Kumpandisha cheo Simbu – kutoka sajini hadi kuwa sajinitaji. Hili likanifurahisha kidogo.

Yaani vipo vinchi mwanariadha wao amepata dhahabu, vikaamua kuwapa ofa nchi nzima; ya kulala, kunywa na kufurahia medali ya dhahabu – hata kama ni kwa gharama zao.

Sisi tumebung'aa. Sijui tukoje, kha!

■ Habari Kuu

# Utafiti: Rais Samia anaaminika zaidi



*Rais Samia Suluhu Hassan*

**Na Mwandishi WETU**

MWEZI mmoja kabla ya kupulizwa kwa kipyenga cha kuanza kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Tanzania wa 2025, ilibainika kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anaaminika zaidi miongoni mwa viongozi wa vyama vya siasa.

Kampeni za kuwania nafasi za rais, wabunge, wawakilishi na madiwani zilianza Agosti 28 na zitamalizika Oktoba 28.

Utafiti huo uliofanywa kwa kipindi cha zaidi ya miezi miwili; kuanzia Januari 22 hadi Machi 28, na kuhusisha mikoa 10 ya Tanzania Bara na miwili ya Zanzibar, ulifanywa na wataalamu wa utafiti kwenye maeneo ya uchumi, siasa, habari na maendeleo ya jamii.

Mikoa iliyohusika kwenye utafiti huo ni Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Geita, Rukwa, Dodoma, Katavi na Mbeya. Kwa upande wa Zanzibar; Kaskazini Pemba na Kusini Unguja.

Katika utafiti huo, sampuli za watu 2,200 zilichukuliwa maoni yao. Watanzania 200 walichukuliwa katika mikoa ya Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar walichukua watu 100 kwa kila mkoa.

Inaelezwa kuwa kwenye utafiti huo, idadi yote ya watu hao, wanawake walikuwa 791 na wanaume walikuwa 1,409. Kwamba watafiti walizungumza na watu wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 61.

Kwenye utafiti huo, kiwango cha elimu hakikuzingatiwa, huku kipato cha mtu hakikuulizwa wala dini haikuwa sehemu ya hojaji utafiti huo.

Akizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki, Paschal Rwemugize, ambaye amejitambulisha kuwa mwenyekiti wa jopo la watafiti hao alisema kuwa viongozi wa vyama vitano vya siasa, ndiyo walikuwa kiini cha utafiti ambapo wananchi waliulizwa maswali kadhaa kuhusu wanavyoaminika kupewa kuongoza Tanzania.

Viongozi wa vyama vya siasa waliohusishwa ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dorothy Semu wa ACT Wazalendo, Tundu Lissu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Hashimu Rungwe wa Chama cha Ukombozi wa Umma (Chaumma) na Profesa Ibrahim Lipumba wa Chama cha Wananchi (CUF).

Wakati wa utafiti huu, vyama vyote havikuwa vimetangaza wagombea wao, isipokuwa CCM ambayo ilitangaza siku tatu kabla ya utafiti huo kuanza.

Miongoni mwa maswali waliyoulizwa ni pamoja na nani anaaminika zaidi kukabidhiwa kijiti cha uongozi wa Tanzania kwenye uchaguzi ujao? Nani anaweza kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili wananchi? Nani anaweza kuwatetea wanapokumbwa na madhila ya uonevu kutoka baadhi ya taasisi za serikali?

Katika utafiti huo uliofanywa kwa njia za kisasa za kukusanya maoni, ikiwamo matumizi ya vishikwambi, haukulazimisha mtu aliyefikiwa na kwamba waliohusika hakuna aliyelazimishwa wala kushawishiwa kwa njia yoyote ile.

Inaendelea Uk. 7

# Utafiti: Rais Samia...

Inatoka Uk. 6

“Sisi tuliamua kufanya utafiti huu kwa hiari kwa kila aliyefikiwa, wapo baadhi waligoma, hawakupenda kutoa maoni yao, na wapo waliojibu maswali kadhaa na wengine kuacha baadhi,”alisema Rwemugize.

Alipoulizwa nani alifadhili utafiti huo, Rwemugize alisema kuwa walipewa kandarasi hiyo na Taasisi ya HumanGauge, ambayo hakuwa tayari kusema ilifanya hivyo kwa kulipwa na nani.

Swali kutoka Pambazuko: Je, ni CCM ndiyo walikupa kazi hiyo? Alikataa katakata, akieleza kuwa endapo wangekuwa CCM au hata serikali, hakuwa tayari kuchukua kandarasi hiyo.

“Matokeo ya kupewa kazi na chama tawala na hata serikali, mara nyingi lazima yatakuwa yamebeba maagizo ya upendeleo, lakini hii ilikuwa kazi ya kitaasisi na binafsi zaidi,” alisema.

Rwemugize alisema kuwa malengo ilikuwa kupata majibu ya imani ya wananchi kuhusu viongozi wao wa vyama vya siasa, ambavyo ukiondoa CCM, ni mbadala wa kuingia Ikulu na kuongoza Tanzania.

Amesema kuwa maelezo ya ziada yaliyokusanywa na kufanyiwa upembuzi na watafiti yanaonyesha kuwa Rais Samia aliibuka kidedea kwa kuaminika kwa kuwa baada ya kuingia madarakani, Machi 19, 2021 ameweza kufanya baadhi ya mambo ambayo yanaonekana na kuneemesha wananchi wengi.

**Mafanikio ya Rais Samia**

Katika kipindi chake, Rais Samia amehakikisha kuna ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya kwa maeneo mengi ya Tanzania.

Rais Samia katika kipindi chake kumekuwepo na ongezeko la hospitali 11, vituo vya afya vinane na zahanati 41.

Kipindi cha miaka inayokaribia mitano akiwa madarakani, Rais Samia amehakikisha kuwepo kwa mtandao mrefu wa usafirishaji na usambazaji wa majisafi kutoka kilomita 3,016 hadi 6,608.

Ni katika muda huo, amewezesha kukamilika kwa kituo kikubwa cha baishara na usafirishaji kwa nchi za Afrika Mashariki. Kituo hicho kiko Ubungo, Dar es Salaam.

Inaendelea Uk. 8



Habari

# Utafiti: Rais Samia...

Inatoka Uk. 7

Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Rais Samia kuwa madarakani, amesimamia na kuhakikisha kuwa vijiji vyote vya Tanzania vinafikiwa na umeme.

**Kampeni kusaka urais zaendelea**

Ikiwa imeingia wiki ya tano sasa tangu kampeni za uchaguzi mkuu zilivyoanza, mikutano ya wagombea urais wa vyama vingine imeonekana kutokuwa na hamasa, ikihudhuriwa na watu wachache.

Tangu alipozindua kampeni zake za uchaguzi mkuu Agosti 28, 2025, tayari Rais Samia amefanya mikutano katika mikoa 17 huku kwa siku akifanya mikutano hadi mara tatu.

Ufuatiliaji wa Pambazuko umebaini kuwa mgombea wa CCM, Rais Samia amekuwa akijinadi kwa kuonyesha mambo yaliyofanywa na chama chake, na huenda hii ikawa kete nyingine inayompa nafasi ya kuaminika zaidi.

Mtwara Mjini

Septemba 26, 2025 akiwa Mtwara Mjini, Samia aliahidi kuwa serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa itakayounganisha Mtwara, Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga mkoani Ruvuma katika miaka mitano ijayo.

Alisisitiza kuwa reli hiyo itakuwa kichocheo cha mageuzi ya kiuchumi kwa mikoa ya kusini na taifa kwa ujumla.

**Lindi**

Akiwa Mchinga mkoani Lindi, Septemba 25, 2025, Samia aliahidi kwamba serikali yake italenga kuhakikisha kila kijiji cha Mchinga kinapata huduma ya majisafi kupitia mradi wa maji wa awamu ya pili.

“Tunaahidi kuendelea kutatua changamoto ya maji Mchinga. Tunajua kazi nzuri iliyofanyika kwenye awamu ya kwanza, lakini mradi wa maji hapa Mchinga una awamu ya pili…”

“Mradi huu utakwenda kufaidisha vijiji vingine 10 vya Mchinga ambavyo bado havijapata maji. Lengo letu ni kuona kila Mwanamchinga anafaidika na maji safi na salama,” alisema.

**Ruvuma**

Septemba 23, 2025, akiwa Tunduru, Ruvuma aliwahakikishia wananchi kuwa serikali inaendelea kufanya mazungumzo ya kimataifa ili kulinda bei za mazao ya kilimo hasa ufuta na mbaazi yasishuke kupita kiasi.

“Kuna miaka bei inapanda juu na kuna miaka inashuka kidogo. Sasa tumezalisha kipindi ambacho na wenzetu duniani wamezalisha kama sisi ufuta, mbaazi na kadhalika, hivyo wametushushia bei kidogo…” alisema.

**Zanzibar**

Akiwa Zanzibar alifanya mikutano katika mikoa yote mitano huku akionyesha namna alivyotekeleza ilani kwa vitendo kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Miongoni mwa ahadi alizotoa ni pamoja na kujenga kituo cha kisasa cha kumbukumbu na nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kitakachosaidia vijana wanaotoka nje ya nchi waujue una maana gani.

Akiwa Pemba, Rais Samia aliahidi endapo akichaguliwa atahakikisha Uwanja wa Ndege wa Pemba unajengwa na kukamilika kwa kiwango cha kimataifa na utakuwa na urefu wa kilomita 2.5. Ahadi nyingine aliyoitoa katika eneo hilo ni kujenga Bandari ya Wete kutokana na mkopo kutoka nchini Korea Kusini na kwamba hadi sasa ujenzi wake unaendelea.

Ahadi nyingine aliyoitoa ni ujenzi wa barabara saba kwa kiwango cha lami Pemba na tayari fedha zake zote zipo.

Akiwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa, Rais Samia amefanya mikutano 11 ya kampeni.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia ameahidi kuendeleza sekta ya kilimo, ujenzi wa viwanda, kuimarisha huduma za kijamii na kuinua wajasiriamali.

Katika sekta ya kilimo, Samia amewahakikishia wakulima kuwa CCM ikiingia madarakani katika miaka mitano mingine itaendelea kuwapatia wakulima mbolea ya ruzuku, viwatilifu na mbegu ili wakulima waendelee kulima kwa tija.

Mikoa mingine ambayo tayari Rais Samia amefanya mikutano ya kampeni ni pamoja Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Tabora, Kigoma na jana ameanza mikutano katika Mkoa wa Pwani.

# Vyama vya upinzani 'vyakata pumzi'

**Na Mwandishi WETU**

ZIKIWA zimemalizika siku 31 tangu kuanza kwa kampeni za uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu, picha halisi ya kile wanachokifanya wagombea katika kampeni imeonekana.

Kwa wapigakura, mwelekeo wa kampeni za urais, ubunge na udiwani uko bayana, kupitia mikutano ya hadhara, ripoti za vyombo vya habari, matangazo na mabango; njia kuu zinazotumiwa na wagombea kuwafikia wapiga kura.

Katika kampeni hizo, Pambazuko linaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa wagombea na vyama vyao, hasa wale wa urais kupitia vyama 17 vilivyotajwa kushiriki uchaguzi mkuu.

Vyama hivyo ambavyo vingi kati ya hivyo, pamoja na kusimamisha wagombea urais, vimeonekana kusuasua na pengine kukwama kabisa kufanya kampeni kutokana na ukosefu wa fedha.

**Mabango**

Katika ufuatiliaji uliofanyika kufikia wiki hii, vyama vya upinzani vimebainika kukwama kuweka mabango ya kuwanadi wagombea wao.

Kutoka kaskazini hadi kusini, magharibi hadi mashariki, kati na maeneo yote ya nchi, mabango yaliyotawala kila kona ni ya wagombea wa chama kimoja, Chama Cha Mapinduzi (CCM).



*Mgombea urais wa AAFP, Kunje Ngombale Mwiru*

Mabango ya CCM yanawanadi wagombea wao; urais na mgombea mwenza, wagombea ubunge na wagombea udiwani.

Ni wazi kuwa katika hili, vyama vingine vimekuwa vikishuhudia kuwa wasindikizaji, kutokana na kushindwa kufanya kampeni kulingana na ratiba inavyoonesha.

Pia, vyama hivyo vimeshindwa kumudu kufanya kampeni ya matangazo redioni, kwenye televisheni, mabango makubwa barabarani, hasa kwenye barabara kuu na mitaani.

Mfanyabiashara na mkazi wa Sinza, Dar es Salaam, Frank Minja, anasema katika hali inayoonekana kwa mwelekeo wa kampeni ulivyo, haoni kama kuna ushindani wowote unaotoa nafasi kwa wapigakura kuchuja, kwa kuwa hadi sasa hata wagombea wa urais wa vyama vingine hawajulikani.

Anasema ni jambo la kushangaza kwamba mgombea anayeonekana kila kona ni mmoja, wa chama tawala CCM, ambaye amekuwa madarakani kwa nafasi mbili za juu kwa miaka kumi sasa, hivyo tayari anajulikana vyema na wananchi wote.

"Mimi hadi sasa tunavyozungumza, sijabahatika kukutana na mgombea mwingine wa urais zaidi ya mgombea mmoja, ambaye ninamfahamu nyakati zote..."

"Hao wengine wanaotajwa sijawaona popote, si kwenye mikutano ya kampeni, kwenye matangazo ya redio, kwenye mabango ya barabarani wala hata mitaani..."

"Kwa hali hii, unaweza kusema kweli kuna ushindani kwenye kampeni za mwaka huu?" amehoji.

Mkazi wa Makumbusho, Dar es Salaam, ambaye pia ni mfanyabiashara, Farid Karsani, anasema anaona kuwa kampeni zinazoendelea ni kama mchezo wa kuigiza, ambao waigizaji ni walewale na kila anapopita anakuta watu walewale.

Inaendelea Uk. 11

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Polisi peaneni busu na haki, siyo uonevu




*Wakili Deogratias Mahinyila*

IELEWEKE kuwa askari wa Jeshi la Polisi, na majeshi mengine, wakiwapenda raia, nao watalipwa upendo na ushirikiano kutoka kwa raia.

Siyo fahari polisi kuchukiwa au kuogopwa na raia. Polisi anayeaminika, hupendwa na raia kuliko kasisi au shehe.

Ifahamike kuwa polisi anayependwa na raia hatafuti taarifa za uhalifu. Yeye huletewa taarifa.

Huko Marekani, wiki chache zilizopita, kijana mmoja akiitwa Tayler Robinson alimpiga risasi na kumuua mwanaharakati Charlie Kirk wakati akihutubia wanafunzi wa chuo kikuu huko Utah.

Kabla FBI hawajafika mbali katika upelelezi, walitangaza dau la dola laki moja (sawa na shilingi za Tanzania milioni 245) kwa mtu atakayesaidia kupatikana kwa muuaji wa Charlie Kirk.

Baba wa kijana anayeaminika kuwa muuaji, alipata taarifa za mtoto wake kuhusika katika mauaji hayo na kumripoti kwa FBI. Kijana alikamatwa mara moja na akakiri kumuua Charlie Kirk.

Baba yake na Tayler Robinson pia ni askari polisi na amefanya kazi hiyo kwa miaka 27. Kwa tukio hili akafanya uamuzi mgumu katika maeneo matatu.

Kwanza, akakataa kupokea dola laki moja zilizotolewa kuwa zawadi kwa atakayesaidia kumpata muuaji wa Charlie Kirk.

Pili, akaamua kujiuzuru kazi ya upolisi kabla ya kustaafu na kukiri kuwa ameshindwa kuwa 'baba mzuri" na mfano kwa mtoto wake.

Tatu, akaahidi kushirikiana na mwendesha mashtaka kuwezesha mtoto wake apate adhabu ya kifo.

Mzee huyo akakiri kuwa aliamua kufanya hivyo ili kuonyesha mfano kuwa askari polisi au jeshi lote, ni rafiki wa haki.

Mwaka 1964, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alivunja jeshi lililokuwa limerithi kila kitu kutoka kwa wakoloni, likiitwa KAR, baada ya kuasi na akaunda JWTZ.

Mwalimu Nyerere alikiri baadaye kuwa jeshi lile liliasi kwa sababu "lilikuwa bado na sura na kasumba ya kikoloni" ndani ya taifa lililo huru.

Maana yake ni kwamba wakoloni waliondoka nchini kwetu wakiwa wameacha jeshi lenye tabia yao.

Kumpiga raia; mpigakura, mlipakodi, mlinzi wa taifa, na mwajiri wa polisi, ni kuasi, ni kunyea mbeleko au mtoto kung'ata titi la mama.

Kwa kuwa wanaopiga inaonekana wanapenda kupigapiga, adhabu yao ni kuzuiwa kupiga.

Katika taifa huru, ni heri polisi kupigwa na raia kuliko kumpiga raia asiye na hatia. Kama ana hatia apelekwe mahakamani akapigwe kwa haki. Hiyo itafundisha vizuri.

Bado kuna muda wa kurudi mezani. Tufanye hivyo sasa.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***

# Vyama vya upinzani

Inatoka Uk. 9

Anaeleza kuwa kila anakopita anaona mabango na kusikia matangazo ya chama kilekile na mikusanyiko ileile, huku wagombea wa vyama vingine hawaonekani kufanya kampeni popote.

"Mimi ni mfanyabiashara na ni mtembezi kweli kutokana na aina ya wateja wangu, nimezunguka Dar es Salaam karibu yote sijaona picha wala bango la mgombea mwingine yeyote wa urais zaidi ya mgombea kupitia CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, mabango yake yako karibu kila barabara na kila kona kwa ukubwa tofauti..."

"Ikija kwa wabunge na madiwani, unakutana na mikutano ya wabunge na madiwani wa CCM tu, purukushani zao na mabango yao kila kona, ndio wanatanda..."

"Kwa picha chache za upinzani zilizopo ni kama vipeperushi kwenye vikaratasi ambavyo vimemezwa na mabango makubwa ya wana CCM..."

"Huu uchaguzi umekuwa mithili ya mechi ya mpira ambayo wachezaji wa timu zote mbili wanafungia goli moja na pointi zote zinaenda kwa timu moja tu..."

"Wagombea wengine wanaonekana kama hawana muda wa kuweka picha zao. Ni kama wanakula fungate la kuzurura tu kwenye maeneo ya nchi wanayoweza kuyafikia kwa magari ya kifahari waliyopewa," anasema.

**Maelezo ya viongozi wa vyama**

Katibu Mkuu wa UPDP, Hamadi Ibrahim anasema wanatambua umuhimu wa kuwanadi wagombea wao kupitia matangazo, mabango ya barabarani na vipeperushi, ila wanakwama kutokana na uwezo mdogo wa kifedha.

Ibrahim ambaye chama chake cha UPDP kimemsimamisha mgombea wa urais, Twalib Kadege, anasema wamechapisha mabango machache na vipeperushi kulingana na uwezo wao kifedha.

Anasema chama kimechapisha mabango ambayo yamewekwa kwenye gari ya mgombea wao wa urais, yakionesha picha yake na mengine yamesambazwa mitaani kwa ajili ya kuomba kura kwa wananchi.

"Kwa suala la mabango, yapo lakini siyo makubwa kama hayo mnayoyaona ya mgombea tunayeshindana naye, wa CCM.."

"Tumechapisha kulingana na uwezo wetu. Gari ya mgombea wetu ina mabango na mengine tumeyapeleka mikoani kwa ajili ya kumtambulisha mgombea na kumuombea kura,"anasema.

Katika mazungumzo yake na Pambazuko, Katibu Mkuu wa chama cha AAFP, Rashid Rai, anasema katika suala hili la kuchapisha na kusambaza mabango, bajeti yake ni kubwa ambayo chama chake hakiwezi kuimudu.

Anasema kuwa wao wameamua kuelekeza nguvu zao za matangazo kwenye maeneo wanayoweza kufika kwa urahisi na bila gharama kubwa.

"Kwa ufupi si kwamba sina mabango, ninayo ya mgombea wangu ila ninatembea nayo kwenye gari na kusambaza machache kwa wananchi kila ninapofanya mikutano.

"Kwa kuwa chama changu ni cha wakulima na kampeni zangu ninafanyia huku pembezoni na mashambani, tunaendelea kuwafikia watu wetu kwa shida kutokana na ukata lakini tunaendelea kuchangishana na kampeni zinaendelea," anasema.

Haya yanaendelea wakati vyama vya siasa 18 vilivyosajiliwa na kufanikiwa na kusimamisha wagombea kwa nafasi za urais, ubunge na udiwani vikiendelea na kampeni kuelekea Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 29 mwaka huu.



*Mgombea urais wa Chama cha The United People's Democratic Party (UPDP), Twalib Ibrahim Kadege.*

Habari/Tangazo

# Chaumma wazidi ‘kujimwambafai’

Na Mwandishi WETU

PILIKAPILIKA za kuingia Ikulu kuongoza Tanzania, zinaendelea kupamba moto, huku kila mgombea urais akijinadi “kuleta maisha bora kwa wananchi.”

Mgombea urais kupitia Chama Cha Ukombozi wa Umma (Chaumma), Salum Mwalimu amesema kuwa “amebeba dawa” ya kumaliza au kupunguza zaidi matatizo” ya wananchi.

Ameeleza kuwa akiwa Rais wa Tanzania, atahakikisha kuwa tatizo la ukosefu wa ajira nchini humo, linakuwa historia.

Oktoba 29, mwaka huu, Watanzania wenye sifa za kupiga kura watachagua viongozi wao; rais, wabunge, wawakilishi (Zanzibar) na madiwani.

Akizungumza katika mikutano yake, mgombea huyo amesema kuwa uwezo wa kufanya hivyo anao na kwamba Tanzania haina upungufu wa ajira, isipokuwa tu viongozi waliopo sasa, wameshindwa kujiongeza na kuwa wabunifu.

Akizungumza wiki iliyopita katika maeneo kadhaa ya Nyakanazi Wilaya ya Biharamulo, Kagera, akiwa njiani kuelekea mkoani Kigoma, Mwalimu amewahakikishia Watanzania kwamba anaweza na kuomba wampe ridhaa hiyo ili wahakikishe anayoahidi.

Amesema kuwa akiwa rais atahakikisha kuwa Tanzania inakuwa na uchumi jumuishi katika sekta na kada mbalimbali, ili kuweza kondoa tatizo la ajira nchini humo.

Mgombea huyo ameongeza kuwa, kupitia sera yake ya kilimo, atahakikisha mazao ya kimkakati kama vile kahawa na pamba, yanatengenezewa mazingira bora ya kuzalishwa na kupatikana kwa masoko ya uhakika yatakayokuwa yananufaisha wananchi.

Mwalimu amekuwa akieleza kuwa chama chake cha Chaumma, kimejipanga “kuwaomboa Watanzania ambao, anadai hawana sababu ya “kuteseka” kwa kuwa nchi hiyo ina kila aina ya rasilimali kuifanya kuwa tajiri.

Katika uchaguzi huo mkuu, Tume Huru ya Uchaguzi Tanzania (INEC), imeeleza kuwepo kwa vyama vya siasa 18 ambavyo zinashiriki katika huo, ingawa vyama vikuu vya siasa havitashiriki; Chama cha Demokrasia na Maendeleo na ACT Wazalendo.



## TANZIA TANZIA

**Gazeti la Pambazuko, linaungana kwa masikitiko katika kuomboleza kifo cha Mzee Benjamin Jacob Bagonza (86), baba mzazi wa Askofu Benson Bagonza, kilichotokea Septemba 29, 2025.**

**Pia, Askofu Bagonza amefiwa na dada yake, Dora Bagonza (64), siku tano baada ya kifo cha baba yake.**

**Uongozi, wahariri, waandishi wa habari, watendaji wengine na wasomaji wa Pambazuko, wanaungana kwa pamoja kuwapa pole familia ya Askofu Bagonza, ndugu, jamaa na marafiki kwa misiba hii.**

**Tunawatakia pumziko la heri ndugu zetu hawa waliotangulia mbele za haki.**





Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Buriani mpenda haki Askofu Munga

KUNA neno ambalo nilikuwa nalisoma katika Biblia ambalo udhahiri wake niliupata asubuhi ya Septemba 20,2025, nilipopokea taarifa ya kifo cha Baba Askofu Stephen Munga.

"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake."

Kama Baba Askofu angejua muda wake au siku yake nisingepokea ujumbe saa 3.56 usiku saa chache kabla hajafariki, kuwa nitakuwa kwenye orodha ya kuombewa na kundi lake la maombi.

Kama ningejua Baba Askofu hatakuwepo tena kabla ya kikao kitakachofuata, baada ya kile tulichoonana mara ya mwisho Dodoma, ningemwuliza maswali mengi.

Nilishtuka nikakumbuka nilipopata kumfahamu Baba Askofu Munga alipoingizwa kazini kuwa askofu wa tatu wa Dayosisi ya Kaskazini Mashariki ya Kanisa la Kiinjili la Kiluteri Tanzania mwaka 2001.

Mara kadhaa nimeisikia sauti yake ya haki na kuna wakati tulikutana katika kongamano la katiba lililoandaliwa na Jumuia ya Kikristo Tanzania (CCT) na niliona utofauti wake katika kujenga hoja kuhusu haki.

Kwa takribani miaka 20 akiwa askofu nilimsikia akikemea maovu, ikiwemo rushwa, uonevu na uvunjaji wa haki.

Alihudhuria midahalo na makongamano yaliyokuwa yakihoji hali ya haki na uvunjwaji wa haki.

Baba Askofu Munga alikuwa mtu mnyofu, aliyekuwa na sauti iliyofanana na wadhifa wake hata pale alipokuwa anaongea jambo gumu linalogusa.

Tuliposhuhudia uvunjwaji mkubwa sana wa haki katika maeneo ya migodini na hata tulipokuwa tunahoji mikataba ya serikali na makampuni makubwa ya migodi ambayo ilitia shaka, sauti ya Askofu Munga ilikuwepo.

Askofu Munga alipostaafu hakukaa kimya aliendeleza msimamo wake wa kuongea haki na kushauri haki.

Sikushangaa aliponishirikisha nia yake ya



Askofu Munga

kuanzisha shirika ambalo alipata maono liwepo kujenga haki, amani na usuluhishi/upatanishi.

Pamoja na changamoto katika uanzishwaji wa shirika hilo hatimaye nia ya Baba Askofu ya kuanzisha shirika litakalosimamia haki, amani na usuluhishi ilifanikiwa na lilianza kazi na linaendelea kujenga uwezo wa jamii katika maeneo hayo muhimu.

Matendo ya huruma alionyesha wazi na ndiyo maana akishirikiana na mwenza wake Mchungaji Dkt. Anneth Munga, alianzisha kikundi cha kuomba, kuombewa, na kuombeana.

Kila siku amekuwa na kikundi ambacho ni cha maombi akiombea watu wasiopungua 70 kwa kuwataja majina yao.

Kundi hilo linaloendelea kwa njia ya mtandao limekuwa na maana sana hasa katika kipindi hiki na wakati watu wanapokutwa na magonjwa na hali ngumu.

Nitaikumbuka sana siku ya mwisho niliyoonana na Askofu Munga kule Dodoma katika kongamano la kujadili hali iliyopo nchini kwa wakati huu ili kutafuta njia sahihi ya kuibadili hali hii.

Alichokisimamia ni kuwa inabidi wote tunaojali kuona haki tusimamie ukweli na kupanga mikakati thabiti bila hofu kukabili yanayoendelea nchini.

Mbegu njema aliyoipanda Baba Munga itaendelea kuota na ipo siku mti wa haki, amani na upatanishi utasimama wima nchini kwetu.

Apumzike kwa amani, baba mpenda haki na msema kweli Askofu Munga.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

■ Habari

# Jeshi la Polisi lazidi kuandamwa




*Mkuu wa Jeshi la Polisi, Camillus Wambura*

**Na Mwandishi WETU**

JESHI la Polisi Tanzania ambalo jukumu lake kubwa ni kulinda raia na mali zao, limeendelea kushutumiwa kwa askari wake kukiuka sheria na miiko ya kazi.

Shutuma hizo zinaelekezwa kwa baadhi ya askari ambao wamekuwa wakibambikia makosa raia wasiokuwa na hatia na kusababisha wananchi hao kuadhibiwa na mahakama kwa makosa ambayo hawakuyatenda.

Askari polisi wengine wamekuwa wakituhumiwa kudai na kupokea rushwa, pia wapo wanaokutwa na hatia mahakamani kwa kukutwa na makosa ya mauaji, ujambazi na hata utekaji.

Kutokana na matukio hayo na mengine, wananchi wamebainika kupoteza imani na askari kwa sababu badala ya kulinda raia, wao wamekuwa wakitumika kuwanyanyasa wananchi.

Moja kati ya matukio ya aina hiyo ya hivi karibuni ambalo limezua mjadala mkubwa kwenye jamii ni baadhi ya askari polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, kuwapiga wananchi waliofika Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Saalam, kufuatilia mwenendo wa kesi ya uhaini inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu.

Baadhi ya watu waliozungumza na Pambazuko wamebainisha kuwa kupigwa kwa wananchi hao ni mwendelezo wa unyanyasaji wa polisi dhidi ya raia kwani kabla ya tukio hilo la Mahakama Kuu, wananchi wengine walipigwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam walipokuwa wakifuatilia kesi hiyo hiyo ya Lissu katika hatua za awali.

Akizungumzia jeshi hilo, Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari, Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (Misa-TAN), Edwin Soko, alionyesha kushangazwa na askari wanaopiga wananchi katika mazingira yasiyokuwa na vurugu.

"Hilo suala la askari polisi kuwapiga raia haliko sawa kabisa kwa sababu hawana mamlaka kisheria kujichukulia sheria mkononi kwani wanazuiwa kisheria kuwapiga raia wasiokuwa na hatia hasa pale wanapokuwa hawajafanya kosa lolote..."

"Kwa kifupi, vitendo hivyo havitakiwi kufumbiwa macho kwani kinachofanywa na polisi wetu ni kuingilia uhuru wa mahakama wakati hawatakiwi kufanya hivyo," alisema Soko.

Pia, aliwataka polisi wote waliohusika kuwapiga wananchi hao mahakamani, wawajibishwe kama inavyotokea nchini Kenya ambako kila askari polisi anayefanya kazi kinyume cha sheria, anawajibika kwa kuchukuliwa hatua.

"Pamoja na hayo, sisi kama Misa-TAN, tunashauri Tanzania tuwe na chombo maalum kinachosimamia Jeshi la Polisi kama ilivyo nchini Kenya ambako wana chombo kinachoitwa IPOA ambacho kazi yake ni kulimulika jeshi hilo na kuwachukulia hatua askari wote wanaokiuka taratibu na sheria zao za kazi," alisema.

**Inaendelea Uk. 15**

# Jeshi la Polisi...

Inatoka Uk. 14

Pia aliliasa Jeshi la Polisi lifanyiwe maboresho ili mkuu wa jeshi hilo na wakuu wengine wa vitengo vya jeshi hilo, wawe wanaomba nafasi hizo kulingana na sifa zao ili kuwafanya wawe watumishi wasioegemea upande wowote kama ilivyo sasa.

**TEF wazungumza**

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alilaani kitendo cha askari polisi kuwapiga raia na kusema kinatakiwa kukoma ili kuendelea kulinda heshima ya jeshi hilo.

"Mahakama ni chombo huru na hakitakiwi kuingiliwa na mtu yeyote kwani wananchi wana haki ya kuhudhuria kesi mahakamani bila kubughudhiwa na bila kujazwa hofu yoyote ile..."

"Binafsi najiuliza askari polisi huwa wanafuata nini mahakamani wakati watuhumiwa wanapelekwa mahakamani na askari magereza..."

"Pamoja na haki waliyonayo wananchi, wananchi haohao nao hawatakiwi kujitoa ufahamu kwa kupigana wala kuwarushia ngumi polisi pindi inapotokea hali ya kutoelewana mahakamani kwa namna yoyote ile," alitahadharisha Balile.




*Askari polisi wakimdhibiti mwanachama wa Chadema aliyejitokeza kusikiliza kesi ya Mwenyekiti wao Tundu Lissu mahakama ya Kisutu jijini Dar es Salaam hivi karibuni.*

**Jowuta wanena**

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania (Jowuta), Musa Juma, alilaani tukio hilo na kuitaka serikali ikemee vitendo vya kikatili vilivyofanywa na askari polisi dhidi ya wananchi wasiokuwa na makosa.

"Sisi Jowuta tunasema sheria na taratibu za kufanya kazi lazima ziheshiwe na askari polisi kwani hao wananchi waliopigwa kwa sababu walikwenda mahakamani, walionewa waziwazi.

"Tunashauri Serikari kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, wakemee tukio hilo kwani vitendo vya askari polisi kuwapiga wananchi na wakati mwingine kuwapiga waandishi wa habari, vinataka kuwa vya kawaida kwa siku za hivi karibuni..."

"Yaani, kama tusipochukua hatua, naamini ipo siku hali itakuwa mbaya zaidi kwani utafika wakati wananchi nao watachoka kupigwa na kuamua kujibu mapigo, jambo ambalo linaweza kutuvurugia amani ya nchi yetu," amesema Juma.

**Kituo cha Demokrasia**

Makamu Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Dorothy Semu, aliwataka askari polisi kutumia mafunzo waliyopata vyuoni kwa kuwadhibiti raia bila kuwapiga.

"Sisi tunaamini polisi wana mafunzo ya kutosha na wamebobea katika kudhibiti raia. Kwa hiyo, watumie mafunzo hayo ipasavyo bila kuwapiga raia kwani wanachokifanya kwa kuwapiga wananchi wasiokuwa na silaha ni uonevu usiokubalika.

"Wasiwapige wananchi, bali watuambie wanaoteka watu, wanapoteza watu na wanaoua watu ni akina nani na wanachukuliwa hatua gani," amesema Semu.

**Jeshi la Polisi**

Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, Naibu Kamishna wa Polisi, David Misime, alipotafutwa ili kuzungumzia matukio hayo, simu yake iliita bila kupokewa, hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi, hakuujibu.

Hata hivyo, mara nyingi jeshi hilo, kupitia kwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro amekuwa akikanusha askari wake kushambulia raia, huku akikemea kuwa "jeshi litamshughulia yeryote anayechezea askari wetu."

■ Makala

# ACT Wazalendo na kitendawili cha wagombea urais


Luhaga Mpina

Na Mawandishi WETU

WAKATI kampeni za uchaguzi mkuu zikiwa zinaingia hatua za mwisho mwisho, Chama cha ACT Wazalendo bado kipo mahakamani kupigania haki ya mgombea urais wake kushiriki.

Ipo hatari kuwa mwaka huu nao chama hicho kikakosa mgombea urais kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu uliopita.

Iwapo mahakama itatupilia mbali kesi hiyo, itakuwa kipindi cha miaka kumi sasa kwa ACT -Wazalendo kushindwa kuwa na mgombea urais.

Siyo kwamba chama hicho kinaamua kutosimamisha mgombea kabisa, lakini mara zote hizo, mizengwe ya kisiasa kutoka ndani na nje ya chama inasababisha hali hiyo.

Mwaka huu ACT Wazalendo kimemsimamisha Luhaga Mpina, ambaye alihama kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika dakika za lala salama kuelekea mchakato wa uteuzi wa wagombea urais na kujiunga na chama hicho cha upinzani.

Kitendo hicho cha kuhama katika dakika za mwisho ndicho kinamkwamisha Mpina hadi hivi sasa kuorodheshwa kuwa mmoja wa wagombea wa nafasi hiyo ya kutaka kuongoza Tanzania.

Mpina ni mwanasiasa wa tatu kupitishwa na ACT Wazalendo kuwania urais tangu kuanzishwa kwake mwaka 2013.

Mgombea wa kwanza alikuwa Anna Mghwira, aliyekiwakilisha chama hicho katika uchaguzi mkuu wa 2015 na baadaye akafuatiwa na Bernad Membe ambaye alipitishwa na ACT Wazalendo kuwa mgombea urais wake katika uchaguzi wa 2020.

ACT Wazalendo kilipata usajili wa kudumu Mei, 2014 na kwa mujibu wa tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) – kabla haijabadili jina na kuwa Tume Huru ya Uchaguzi (INEC), mwaka 2015 Mghwira alipata kura 323,112 nchi nzima.

Membe ambaye aliwahi kuwa waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na kachero mbobezi, baada ya kuteuliwa kugombea urais hakufanya kampeni na kusababisha sintofahamu iliyowapa wakati mgumu viongozi na wanachama wa chama hicho.

Tofauti na ilivyotarajiwa, Membe, ambaye alitarajiwa kufanya kampeni za kishindo dhidi ya mgombea wa CCM, John Magufuli na Tundu Lissu wa Chadema, alishindwa kufanya kampeni katika mazingira ambayo yaliwaacha mdomo wazi wanachama na viongozi wa ACT Wazalendo ambao waliamua kubadili "gia angani" na kumuunga mkono Lissu.

Kiongozi wa chama wakati huo, Zitto Kabwe na Maalim Seif Sharif Hamad walitoa tamko kuwataka wanachama wao wote kumuunga mkono Lissu upande wa urais.

Membe alifanya mikutano ya kampeni Lindi Mjini na Rufiji, Pwani pekee na hakuonekana kwa zaidi ya majuma mawili.

Baadaye, alijitokeza kwenye vyombo vya habari na akisisitiza kuwa yeye yungali kwenye mbio za kuwania urais na atafunga bao dakika ya 89 ya mchezo na kuibuka mshindi.

Lakini, licha ya kauli hiyo, Membe hakurejea tena kwenye kampeni. Kwa maana hiyo, kiufundi, unaweza kusema kuwa katika uchaguzi huo ni kama vile ACT Wazalendo hakikuwa na mgombea urais kiasi cha viongozi wake wa juu kutoa waraka wa kumuunga mkono mgombea urais kutoka chama kingine.

Kosa hilo la kiufundi, kwa ACT Wazalendo limejirudia tena mwaka huu ambapo mgombea urais wa chama hicho, Luhaga Mpina, ameondolewa kwenye kinyang'anyiro hicho kwenye hatua za mwisho kutokana na pingamizi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Inaendelea Uk. 17

# ACT Wazalendo...

Inatoka Uk. 16

Kiini cha kuenguliwa kwake ni mwanachama wa ACT Wazalendo, Monalisa Ndalla, ambaye awali alipeleka barua Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, akipinga Mpina kuteuliwa kuwa mgombea urais wa chama hicho kwa maelezo kuwa uteuzi wake ulikuwa umekiuka katiba ya chama.

Hoja za Ndalla zilikubaliwa na msajili ambaye katika majibu yake kwa Ndalla, na nakala kupelekwa INEC, alisema Mpina amekosa sifa za kuwa mgombea urais wa ACT Wazalendo.

Baada ya kupokea nakala ya barua hiyo, INEC ikakiandikia ACT Wazalendo kukifahamisha kuwa Mpina amekosa sifa za kuteuliwa kuwa mgombea urais, hivyo kumpiga marufuku kurejesha fomu za uteuzi ambazo alikuwa amekabidhiwa.

Barua hiyo iliandikwa siku moja kabla Mpina hajarudisha fomu na kweli alipokwenda kwenye ofisi za INEC siku iliyofuata alizuiliwa na askari polisi kuingia kwenye ofisi hizo, hivyo akashindwa kurejesha fomu.

Mpina aliamua kukimbilia mahakamani ambako alipata ushindi baada ya Mahakama Kuu kueleza kuwa INEC ilikosea kwa kumzuia Mpina kurejesha fomu za uteuzi na kuamuru kuwa INEC izipokee fomu hizo na kuzishughulikia kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa kisheria.

Mpina akarejesha fomu INEC na kabla uteuzi wake haujathibitishwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wagombea kadhaa wa vyama vingine vya upinzani, walimwekea pingamizi, huku Mpina yeye akimwekea pingamizi mgombea wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan.

Mapingamizi yote yaliyowekwa na wanasiasa hao yalikataliwa na INEC isipokuwa lile lililowekwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Mpina.

INEC ililikubali pingamizi hilo na kumwondoa Mpina kwenye orodha ya wagombea urais, kwa mara ya pili.

Mpina akakimbilia tena mahakamani kuitafuta haki yake ambako kesi hiyo bado inaunguruma.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema kuwa uwezekano wa mgombea huyo na chama chake kufanya kampeni za tija kwa ajili ya uchaguzi huu ni finyu sana.

Wanasema kuwa hata kama mahakama itamrejesha Mpina, lakini siku za kampeni zitakuwa zimesalia chache sana kiasi kuwa itakuwa vigumu kwa mgombea huyo kuyafikia maeneo mengi nchini kufanya kampeni.

ACT wavurugana

Sintofahamu hiyo ya kukosa wagombea kwa mara ya pili kumesababisha vuguvugu la wazi kwenye chama hicho ambapo baadhi ya wanachama wake akiwamo mbunge wa zamani wa Kilwa Kaskazini, Selemani Bungara, maarufu ‘Bwege’ kuhoji mwenendo huo.

Katika mahojiano aliyoyafanya na vyombo kadhaa vya habari, Bwege amenukuliwa akisema kitendo cha kukosa wagombea urais kwa mara ya pili mfululizo siyo jambo la bahati mbaya.

Anahimiza kuwa suala hilo linampasa kumfanya mtendaji mkuu wa chama hicho - Katibu Mkuu, Ado Shaibu, kujitafakari na kuwajibika kwa kujiuzulu.

Bwege anasisitiza kuwa katibu mkuu wa chama kinachojinasibu kuwa makini kama ACT Wazalendo hawezi kuendelea kubaki ofisini kwa tukio hilo kubwa ambalo linajitokeza kwa mara ya pili mfululizo.

Kwa mujibu wa mwanasiasa huyo, uteuzi wa mgombea urais siyo jambo la ghafla hivyo inashangaza kuwa kwa miaka yote mitano inakuwaje chama hicho kilishindwa kujiandaa kusimamisha mgombea urais hadi dakika za mwisho kusubiri mtu kutoka chama kingine.

Wakati Bwege akisema hayo, Pambazuko linafahamu kuwa kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, alijiandaa vilivyo kuwania nafasi hiyo.

Wapasha habari kutoka ndani ya chama hicho wanasema kuwa takribani safu yote ya uongozi ilikubaliana kuwa Semu ndiye atakuwa mgombea urais wa ACT Wazalendo katika uchaguzi wa mwaka huu, lakini wengi sasa wameshikwa na bumbuwazi nini kimetokea hadi mwanamama huyo akapigwa mkasi na Mpina kuteuliwa badala yake.

Kitendo cha ACT Wazalendo kukosa mgombea urais kwa mara ya pili mfululizo, kunaweza kukiathiri chama hicho ambacho wengi wanaamini kuwa kilikuwa kinaelekea kuwa moja ya vyama vikubwa vya upinzani nchini.



# Ripoti: Tanzania yakua haraka kibiashara Afrika




Na Mwandishi WETU

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazokua kwa kasi kwenye uchumi – unaochochewa na biashara, kwa nchi za Afrika

Hali hiyo inatokana na kuwepo mazingira mazuri ya kufanya biashara – kati ya Tanzania na mataifa mengine, mazingira bora ya uwekezaji na uongozi wa kisiasa unaoimarika.

Ripoti ya DHL Trade Atlas ya mwaka huu -2025, inaonyesha kuwa Tanzania, ikiwa miongoni mwa nchi za Afrika zilizofanyiwa utafiti, sasa inachukua nafasi muhimu katika mipango ya biashara duniani, ikichochewa na bidhaa za kilimo na huduma za usafirishaji, sambamba na juhudi za kuimarisha ujumuishaji wa kikanda.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, biashara ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara inatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 5.3 kwa mwaka kati ya 2024 na 2029, ikilinganishwa na ukuaji mdogo wa asilimia 0.8 kati ya 2019 na 2024.

Tanzania yazidi kuimarika

Kwa Tanzania, ripoti hii inaleta taswira ya matumaini kwani imetajwa miongoni mwa nchi 10 za Afrika zinazokua kwa kasi zaidi katika biashara na uchumi.

Ukuaji huo pia unaelezwa kuimarika na kukua kwa biashara za dhahabu, korosho, kahawa na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya bandari na reli ya kisasa.

Ukuaji wa biashara wa Tanzania kwa kipindi cha 2019–2024 ulifikia asilimia saba, huku makadirio yakionesha kuendelea kwa kasi ya asilimia 8 kati ya 2024–2029.

Ukuaji huu unaifanya Tanzania kuwa kitovu cha kuvutia kwa wawekezaji wa kikanda na wa kimataifa, hususan katika nyanja za usafirishaji na nishati.

Fursa na changamoto

Kwa ujumla, Afrika inajipatia nafasi muhimu kama mtoaji wa malighafi za kipekee zinazohitajika katika mapinduzi ya nishati safi—ikiwemo kobalti, shaba, bauxite na manganese.

Madini haya yanatumika kutengeneza betri za magari ya umeme na teknolojia za nishati safi.

Hata hivyo, changamoto bado zipo ikiwemo kitendo cha kuuza rasilimali ghafi jambo ambalo linauweka uchumi katika hatari ya "kutetereka" hasa kwenye bei ya bidhaa duniani.

Aidha, kuna changamoto ya gharama kubwa za usafirishaji na miundombinu duni.

Kwa mujibu wa tafiti, gharama za usafirishaji Afrika zinaweza kufikia mara tano zaidi kwa kila umbali ikilinganishwa na Marekani, huku gharama za usafirishaji zikiwa kati ya asilimia 40 na 60 juu ya wastani wa dunia.

Mabadiliko ya tabianchi pia ni tishio kubwa hasa katika ukanda wa kusini na mashariki mwa Afrika, ambao unakabiliwa na ukame unaosababisha uhaba wa chakula, na Zimbabwe pekee ikishuhudia upungufu wa mazao ya mahindi kwa zaidi ya asilimia 70 mwaka huu.

**Mtazamo wa kibiashara**

Ripoti ya DHL inaonyesha kuwa ingawa nchi kubwa zikiwamo China na Marekani bado zinaongoza kwa wingi wa biashara na uchuki imara, kasi yao ya ukuaji imepungua.

Katika muktadha huu, nchi za Afrika, ikiwemo Tanzania, zinatumia fursa ya kupanda ngazi kibiashara kimataifa, hata kama bado zina viwango vidogo vya jumla.

Aidha, ukuaji wa biashara ya kidijitali unatoa mwanya mpya kwa kampuni za Afrika kushiriki katika masoko ya kimataifa bila kuhitaji uwekezaji mkubwa wa miundombinu.

Kwa Tanzania, hii ni nafasi ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na madini, kuongeza viwanda vya kusindika na kupanua masoko ya kikanda kupitia Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC).

Hatua hizi zikichukuliwa, taifa linaweza siyo tu kuongeza mauzo nje, bali pia kuboresha ajira na mapato ya serikali.


Watalii wakiwa Mbugani

# Zawadi za Serengeti kutolewa Desemba

Na Mwandishi WETU, Arusha

SERIKALI kwa kutambua umuhimu wa utalii, imekuwa ikitumia njia anuai kuchechemua sekta hiyo ili iwe kubwa na bora zaidi.

Moja ya njia hiyo ni kutambua kuwepo kwa wahusika wanayoikuza na kuwa chachu ya mapato, hivyo kuongeza ustawi wa Watanzania. Utambuzi huo ni kuwapa tuzo na zawadi mbalimbali wahusika hao.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi, amesema kuwa ili kuwaenzi wahusika wa kukuza utalii, Tuzo za Uhifadhi na Utalii maarufu kama Serengeti Awards zitafanyika Desemba 19, 2025 jijini Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari katika hafla ya Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani kwenye Kreta ya Ngorongoro, Jumamosi iliyopita, Dkt. Abbasi alisema tuzo hizo zina lengo la kutambua, kuheshimu na kusherehekea mchango wa wadau mbalimbali katika sekta ya uhifadhi na utalii nchini.

Alifafanua kuwa jumla ya tuzo 56 zitatolewa katika makundi saba ambazo ni kura za wananchi kuonesha ni nani anayetambulika zaidi kwa mchango wake katika sekta hiyo, kampuni na waendeshaji wa shughuli za utalii waliobobea katika ubunifu na ubora wa huduma pamoja na waongoza watalii katika taaluma mbalimbali ikiwamo safari, mlima na utamaduni.

Zingine ni tuzo kwa nyumba za kulala wageni na migahawa bora, taasisi, vikundi na watu binafsi wanaoongoza katika juhudi za kuhifadhi maliasili, taasisi na kampuni zinazojitokeza kuonesha vivutio kupitia maonyesho ya kitaifa na kimataifa, na washirika, taasisi au watu binafsi waliotoa mchango wa kipekee katika sekta ya uhifadhi na utalii.

Dkt. Abbasi alisema dirisha la kupokea maombi ya kushiriki kuwania tuzo hizo litafunguliwa Oktoba 10 hadi 31, 2025 kupitia tovuti rasmi ya wizara: https://serengetiawards.maliasili.go.tz

"Wadau wote wenye sifa wataweza kushiriki na hafla ya utoaji rasmi wa tuzo itafanyika Desemba 19, 2025 jijini Arusha," aliongeza msomi huyo mbobezi kwenye masuala ya sekta ya habari. Awali, alieleza kuwa tuzo hizo zilizinduliwa Desemba 20, 2024 jijini Arusha ambapo pia baadhi ya wadau walitunukiwa tuzo za heshima kwa mchango wao katika kukuza uhifadhi na utalii nchini.

## Ilani za vyama Uchaguzi Mkuu 2025

# Ahadi za vyama sekta ya maji



Na Mwandishi WETU

UPO msemo wa Kiswahili kuwa maji ni uhai. Msemo huu unatokana na ukweli kuwa maji yanahusika kwa kiasi kikubwa katika kuhimili maisha ya binadamu.

Ndio maana sekta ya maji ni muhimu na nyeti kila mahali.

Kutokana na umuhimu wa maji, jamii imeshuhudia jamii na pengine hata nchi, zikiingia katika migogoro kisa tu kugombea maji.

Mfano wa hivi karibuni ni mgogoro kati ya Ethiopia na Misri kuhusiana na matumizi ya maji ya Mto Nile.

Pamoja na kugusa maisha moja kwa moja, maji pia ni muhimu katika maeneo ya afya, uwekezaji, uzalishaji wa chakula na miundombinu.

Ndio maana katika ilani za vyama, suala la maji linapewa kipaumbele kikubwa.

Gazeti la Pambazuko katika mfululizo wa kuchapisha ahadi za vyama – kwa mujibu wa ilani zao, leo tunaangazia sekta ya maji.

Endelea kufuatilia.

**ACT Wazalendo kuwekeza 10tr/-**

Serikali ya ACT Wazalendo imeahidi kuwaondolea wananchi adha ya maji na kuhakikisha kuwa kila Mtanzania atapata maji safi na salama.

Chama hicho kimenadi na kuwahakikishia wananchi kupata maji ya bomba kwa gharama nafuu kwa kuzifikia kaya zote ndani ya miaka mitano.

Serikali ya ACT Wazalendo inaahidi kuwekeza shilingi trilioni 10 ndani ya miaka mitano, wastani wa shilingi trilioni mbili kila mwaka, kwenye kumaliza kabisa tatizo la maji safi na salama kwa wananchi.

ACT Wazalendo ainaahidi pia kutoa maji bure kwa kaya masikini na watu wenye ulemavu wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Aidha, itatoa mikopo ya bei nafuu kwa ajili ya ujenzi wa visima vya maji, kama mpango wa muda mfupi na wa dharura kwa jamii zenye changamoto kubwa ya maji.

Serikali hiyo itatengeneza miundombinu ya majitaka na kuunganisha majumbani katika miji na majiji.

**Chaumma kutenga bajeti ya kutosha**

Serikali ya Chama Cha Ukombozi wa Umma (Chaumma), imeahidi kuwaunganisha Watanzania wote wa mijini na vijijini kwenye mtandao wa maji safi na salama ya bomba.

Ili kufikia lengo hilo, serikali hiyo imeahidi kutenga bajeti ya kutosha katika miradi ya maendeleo ya maji kila mwaka ili kuongeza kasi ya kuwaunganisha Watanzania na mtandao huo.

Kwamba itaanzisha miradi ya kuvuna, kuhifadhi na kufanya matumizi endelevu ya maji ya mvua kwa ajili ya shughuli ya matumizi ya kawaida, pamoja na matumizi ya shughuli za kiuchumi hususan kilimo, mifugo na viwanda.

Chaumma itadhibiti upotevu wa maji hasa maeneo ya mijini ambako husababishwa na uchakavu au ubovu wa miundombinu ya maji.

Katika kukabiliana na changamoto ya maji taka, chama hicho kimeahidi kupima maeneo yote ya makazi na kuunganisha na mfumo wa maji taka nchini ili kukabiliana na magonjwa ya milipuko yanayosababishwa na utumiaji wa maji machafu.

Inaendelea Uk. 21

# Ahadi za vyama...

Inatoka Uk. 20

**UDP kuja na maji salama kwa wote**

Chama cha United Democratic Party (UDP), kitahakikisha kila Mtanzania anapata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi ya nyumbani, kilimo, mifugo, viwandani na huduma za kijamii, mijini na vijijini.

Kitajenga miundombinu ya kudumu ya maji ikiwamo mabwawa, visima, mitambo ya kuchuja maji, matenki, mabomba na mifumo ya umwagiliaji ya kisasa.

Serikali hiyo itakuwa na usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji kwa uhifadhi na kulinda mito, maziwa, chemchem na maji ya chini ya ardhi ili yasikauke wala kuchafuliwa.

Matumizi ya teknolojia na ubunifu – kutumia njia bunifu kama uvunaji wa maji ya mvua, teknolojia za kuchuja na kuhifadhi maji, na mifumo ya kidigitali ya kusimamia matumizi.

**CCM kuwa na Gridi ya Taifa ya Maji**

Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambacho kinapigania kuendelea kushika madaraka, kimeahidi kutekeleza mpango kabambe wa taifa wa maji na kuendelea na utekelezaji wa mtandao wa Taifa (National Water Grid).

Mtandao huo utatumika kusambaza maji kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo kujenga mradi wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Singida na Dodoma.

CCM kimejipambanua na kueleza kuwa kitakamilisha miradi ikiwamo wa miji 28, Kiwira – Mbeya, kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa, mradi wa maji wa Kidunda pamoja na kuchimba visima na mabwawa.

**SAU kugawa maji bure**

Chama cha Sauti ya Umma (SAU), kimedhamiria kutoa huduma ya maji safi na salama bure kwa kaya zote milioni 15 kwa mwaka 2025.

Serikali ya SAU itajenga mabwawa makubwa yanayowezesha kuvunwa na kukusanya maji ya mvua ambayo yatatumika na binadamu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji badala ya maji yote kuishia baharini.

Aidha, miradi mbalimbali itaanzishwa ili kumaliza kabisa tatizo la maji nchini Tanzania.

**DP yaahidi maji bure**

Sera ya Chama cha Democratic Party (DP), ni kuwapatia Watanzania wote maji bure.

Hivyo, chama hicho kimeahidi kuendeleza, kuimarisha na kusimamia upatikanaji wa maji safi na salama kwa kila Mtanzania.

Katika kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kinakuwa cha tija DP kimewaahidi wapiga kura kuwa kitahakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha unakuwepo kwa ajili ya umwagiliaji wa mashamba madogo na makubwa.

DP kitajenga visima virefu na vifupi katika umbali usiozidi mita 300 na kila kisima kitatoa maji mwaka mzima.

**AAFP kujenga gridi ya maji**

Chama cha Wakulima (AAFP), kimewaahidi wapiga kura kuwa kitajenga gridi ya maji ya taifa, kuweka miundombinu ya upatikanaji wa maji safi na salama katika kila kaya na kuweka gharama nafuu kwa wananchi katika upatikanaji wa huduma hiyo.

**ADA-Tadea kuchimba visima virefu**

Chama cha African Democratic Alliance (ADA-Tadea), kimedhamiria kuwachimbia visima virefu wananchi walio mbali na maziwa, pia kuuendeleza mradi wa maji ya Ziwa Viktoria hadi Dodoma kupitia Singida.

Serikali ya chama hicho imeahidi kuwa maeneo yote yaliyo karibu na maziwa ikiwamo Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Mbeya na Ruvuma hayatakosa maji.

Pia, itahakikisha huduma za majitaka zinasambaa kwenye maeneo yote.

**NLD kusogeza maji vijijini**

Chama cha National League for Democracy (NLD), kimeahidi kuwa endapo wananchi watakichagua kushika dola, kitaunganisha zaidi ya vijiji 5,000 kwenye huduma ya maji ya bomba ifikapo mwaka 2030.

Pia, kitajenga visima virefu, mabwawa ya maji ya mvua na vituo vya kuchotea maji karibu na makazi ya watu.

Kimeahidi kulinda na kurejesha vyanzo vya maji ya asili kupitia sheria na uelimishaji jamii.

Wiki ijayo tutaangazia sekta ya madini

■ Maisha




*Mjasiliamali wa matunda ambaye ni mwalimu, Jenister Tesha, akiandaa matunda kwa ajili ya kuuza kama alivyokutwa katika eneo la Makumbusho, Dar es Salaam juzi. (Na Fidelis Felix).*

# Aamua ‘kutupa chaki.’ Sasa anauza matunda

**Na Mwandishi WETU**

KATIKA maisha juhudi na maarifa ndizo nguzo zinazoweza kumfanya mtu afike anapotaka. Pesa ni msingi mzuri, lakini bila kuwa na maarifa ya kuendeleza shughuli fulani, fedha hizo zinaweza zisizalishe na kufikia malengo.

Zipo sababu nyingi ambazo zinaweza kumfanya mtu akate tamaa katika safari ya maisha.

Lakini, katika mazingira kama hayo, mtu anapaswa kuendelea kupambana bila kuchoka ili kufanikisha malengo.

Jenister Tesha ni mfano wa wanawake wapambanaji ambaye maisha yake yamethibitisha kuwa kujituma kunaweza kumkwamua mtu kutoka katika changamoto anazokabiliana nazo.

Kupambana kwake kumemuinua kutoka hatua moja ya mafanikio hadi nyingine.

Katika mahojiano na Pambazuko, mwanamke huyo ambaye maisha yake yamejaa historia, anasema hivi sasa anamshukuru Mungu kutokana na kupata mahali pa kujishikiza.

Anasema kitaaluma yeye ni mwalimu wa shule ya msingi, elimu ambayo aliipata mkoani Singida na kuhitimu mwaka 2002.

Jenister anasema kabla hajamaliza masomo ya stashahada ya ualimu, alipata ujauzito na kujifungua watoto mapacha watatu wa kike.

“Nilipojifungua niliishi Arusha kwa mama yangu mdogo, kwa kuwa nilikuwa mtaalamu wa saluni nilipata kazi saluni nikawa nasuka na kupata riziki...”

“Watoto walipofikisha miaka miwili, nilikuwa nikienda nao saluni na dada wa kazi na kufanya shughuli kisha jioni tunarudi nyumbani,” anaeleza.

Anasema aliwalea watoto hao katika safari yenye shida nyingi kutokana na changamoto za maisha.

Hata hivyo, kutokana na kutokata tamaa, aliweza kuwalea na kuwasomesha watoto hao na hivi sasa wawili kati yao wanasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Jenister, ambaye anajishughulisha na biashara ya kuuza matunda katika eneo la Kijitonyama jijini Dar es Salaam, anasema pacha wake wa tatu ameishia elimu ya kidato cha nne.

Inaendelea Uk. 23



# Aamua ‘kutupa chaki.’

Inatoka Uk. 22

Ingawa kitaaluma yeye ni mwalimu, lakini aliamua kuachana na taaluma yake na kujikita kwenye ujasiriamali kutokana na kazi ya ualimu kutolipa vizuri.

Anasema majukumu ya kulea mapacha watatu yalikuwa yanahitaji fedha nyingi ambazo hakuweza kuzipata akiwa mwalimu.

Lakini mbaya zaidi, alisota bila hata kupata hiyo ajira ya ualimu.

“Nilipoona ugumu huo, niliamua kutupa chaki na kuingia huku kwenye ujasiriamali, naona maisha yangu yanasonga na sasa hivi kwa kweli huwezi kunirudisha tena kwenye chaki,” anasema Jenister.

Anasema kazi hiyo inamwezesha kuwahudumia watoto wake waliopo chuo kikuu kwa kulipa sehemu ya ada - kwa sababu hawakupata mkopo kwa asilimia 100, kulipia pango na gharama nyingine za maisha.

“Nipo sambamba na watoto wangu kwa kila hali, nina imani watakapomaliza, ninaweza kutulia na kukusanya kiasi cha kutosha cha fedha kwa ajili ya kupanua shughuli zangu na kufanya mambo mengine ya maendeleo,” anaeleza.

Anasema aliamua kuanza biashara ya kuuza matunda kutokana na matatizo aliyopitia katika maisha.

Jenister anasema awali alikuwa anafanya kazi ya ususi ambayo haikuwa inamlipa sana.

“Kwa kawaida watu wanadharau baadhi ya kazi, lakini unapokuwa na matatizo kama akili yako inafanya kazi vizuri, hiyo kazi ambayo watu wanaidharau inaweza kuwa ndio mkombozi wako,”anasema.

Anasema aliachana na kazi ya ususi kutokana na matatizo ya kiafya.

Mwanamama huyo akifafanua, anabainisha kuwa hivyo ndivyo alivyoangukia kwenye biashara ya matunda, ambayo watu wengi wanaidharau na kuiona kuwa siyo ya maana sana.

“Lakini amini usiamini, hii ndiyo biashara iliyoniwezesha kuwasomesha watoto wangu hadi ngazi ya chuo kikuu,”anasema.

Anasema wanawake wengi, hasa waliopata elimu nzuri na kushindwa kupata ajira, ‘hawafungui’ akili zao na kuona fursa zilizopo mbele yao...”

“Wengi wamekuwa wakiangalia mambo ambayo wamesomea na kila mara akili yao imejikita kutafuta ajira, tena ya kile kitu walichosomea,”anaongeza.

Anasema watu kama hao wakiamua “kufikiri nje ya boksi,” wanaweza kubaini fursa lukuki ambazo zipo ambazo zinaweza kumletea fedha nyingi kuliko zile ambazo angezipata kwenye ajira. “Nayasema haya siyo kwa kusikia kwa watu, mimi mwenyewe nimeisha maisha ya aina hiyo,” anasema.

Makala

# Nchi tano Afrika upinzani ulikoibuka kidedea



Rais Mokgweetsi Masisi, aliyeshindwa kutetea kiti chake

Na Mashirika ya HABARI

MWAKA mmoja uliopita umekuwa mchungu kwa serikali kadhaa za Afrika zilizo katika eneo la kusini mwa Jangwa la Sahara.

Uchaguzi uliofanyika katika eneo hili, hasa kwenye nchi zinazofuata demokrasia, vyama tawala vilipoteza idadi kubwa ya viti vya ubunge au kuondolewa kabisa madarakani.

Katika kipindi hicho, kumeshuhudiwa mabadiliko katika nchi sita ikiwemo Malawi ambayo Rais Lazarus Chakwera, aliyekuwa anatetea kiti chake, amekubali kushindwa dhidi ya mpinzani wake, Peter Mutharika.

Akihutubia taifa Jumatano iliyopita kabla ya matokeo ya uchaguzi mkuu kutangazwa rasmi, Rais Chakwera aliliambia taifa lake kuwa anafanya hivyo kwa kuheshimu nia yao ya kutaka mabadiliko ya serikali.

Matokeo ya awali kabisa yalionyesha mpinzani wake, rais wa zamani Peter Mutharika, ameongoza vyema, akijizolea karibu asilimia 66 ya kura zilizohesabiwa hadi Jumanne iliyopita. Chakwera alikuwa amepata asilimia 24 tu.

Tanzania, Cameroon, Guinea-Bissau Jamhuri ya Afrika ya Kati ni miongoni mwa nchi zinazokwenda kwenye uchaguzi mkuu kuanzia wiki chache zijazo.

Lakini katika miaka ya hivi karibuni ukiacha Malawi, nchi hizi zingine tano zimeshuhudia vyama vya upinzani vikifanya vyema zaidi dhidi ya vyama vinavyokuwa madarakani.

**Botswana**

Moja ya mambo ya kushangaza zaidi ya uchaguzi uliofanyika mwaka jana, 2024, ambapo ilishuhudiwa kushindwa kwa serikali ambazo hapo awali zilionekana kuwa na nguvu kubwa ya madaraka - ikiwa ni pamoja na nchi ambazo hazijawahi kupata mabadiliko katika uongozi wa juu.

Chama cha Botswana Democratic Party (BDP) ambacho kilikuwa kimetawala nchi hiyo tangu uhuru mwaka 1966, kilisambaratishwa katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka jana.

Pamoja na kupoteza mamlaka, chama cha BDP kilishindwa kufikia idadi ya wabunge 38 kama ilivyokuwa awali katika bunge lenye wabunge 69, na kikakaribia kufutwa kabisa.

Baada ya kushinda viti vinne pekee, BDP sasa ni moja ya vyama vidogo zaidi bungeni na kinakutana na changamoto kubwa ya kubaki na nguvu ya kisiasa.

UDC inayoongozwa na Duma Boko ilionge-za zaidi ya mara mbili ya mgao wake wa viti bungeni- kutoka 15 hadi 36.

Kutokana na hali ya mdororo wa kiuchumi (uliosababishwa kwa kiasi kikubwa na mdororo wa mapato kutokana na mauzo ya almasi), maisha marefu ya BDP na mtindo wa utawala wa Rais Mokgweetsi Masisi uliwakasirisha wapiga kura vijana wakaamua "kukipiga chini"chama hicho katika uchaguzi.

**Senegal**

Kwa upande wa Senegal, mabadiliko ya kisiasa yalikuwa ya kushangaza kama ilivyokuwa nchini Botswana, ingawa kwa njia tofauti.

Majaribio ya rais aliye madarakani kutaka kufanya udanganyifu kinyume na katiba yalikabiliwa na mchanganyiko wa uhamasishaji wa upinzani na uhuru wa mahakama.

Inaendelea Uk. 25

# Nchi tano Afrika...

Inatoka Uk. 24

Pia, maandamano ya mitaani – yaliyokuwa yakifanyika mara kwa mara, yakiongeza shinikizo kwa utawala wa Rais Macky Sall.

Katika maandalizi ya uchaguzi huo, utawala wa Rais Sall ulitumia mbinu mbalimbali kuzuia vuguvugu la vijana maarufu (African Patriots of Senegal for Work, Ethics and Fraternity - PASTEF) linaloongozwa na kiongozi wa upinzani, Ousmane Sonko.

Kufungwa kwa wanaharakati vijana, kwa mfano Sonko mwenyewe na Bassirou Faye, na jaribio la kuchelewesha uchaguzi, kuliashiria hatua ya mabadiliko katika harakati za Senegal kuelekea demokrasia zaidi.

Wiki chache kabla ya uchaguzi, viongozi wa upinzani Bassirou Diomaye Faye na Ousmane Sonko walikuwa wakiteswa gerezani, huku serikali ya Rais Macky Sall ikitumia vibaya mamlaka yake ili kuepuka kushindwa.

Shinikizo la ndani na kimataifa lililosababisha Faye na Sonko kuachiliwa huru Machi 14, 2025, lilimsaidia Faye kushinda urais katika duru ya kwanza, huku mgombea wa serikali akiambulia asilimia 36 pekee ya kura.

**Somaliland**

Jamhuri iliyojitenga na kutambuliwa kimataifa kuwa serikali huru, Somaliland, ilifanya uchaguzi wa amani ambao ulisisitiza madai yake kuwa chombo thabiti cha kidemokrasia.

Chama tawala, Kulmiye - kilichokuwa madarakani tangu 2010 na kinachoongozwa na Rais Muse Bihi Abdi tangu 2017 - kiliwania dhidi ya chama kikuu cha upinzani cha Waddani, ambacho kiongozi wake Abdirahman Mohamed Abdullahi, alipata asilimia 64 ya kura na kuwa Rais wa sita wa Somaliland. Bihi Abdi alipata asilimia 35 ya kura.

Matatizo ya kiuchumi, siasa za kijiografia na siasa za kimila zilifanya iwe vigumu kwa chama kilicho madarakani kuwashawishi wapiga kura kukipigia upatu kuendelea kukaa madarakani.

Ushindi wa Waddani unaonyesha uthabiti wa kidemokrasia wa Somaliland. Na viongozi wote waliahidi kufanya juhudi eneo hilo la Somalia litambulike kimataifa.



*Rais Lazarus Chakwera aliyeshindwa kutetea kiti chake*



*Peter Mutharika*

**Ghana**

Rais wa zamani wa Ghana, John Mahama, ambaye pia alikuwa kiongozi mkuu wa upinzani nchini humo, alishinda tena urais katika uchaguzi uliofanyika Desemba 7, 2024.

Mahama, ambaye aliwahi kuwa rais wa nchi hiyo kuanzia mwaka 2012 hadi 2017, alikiwakilisha chama cha National Democratic Congress (NDC) alimshinda makamu wa rais wa nchi hiyo, Mahamudu Bawumia aliyewakilisha chama tawala cha NPP.

Uchumi kuporomoka, ukosefu wa ajira kwa vijana na mfumko wa bei, ni miongoni mwa hoja ambazo chama cha NDC kilitumia kupata wingi wa wabunge (viti 183 dhidi ya 88 vya NPP).

***Makala haya yamechukuliwa kutoka tovuti ya BBC Swahili na kuhaririwa kidogo kukidhi vigezo vya Pambazuko.***

# Barua za wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Tumechoshwa na usafiri wa mwendokasi

**Mhariri,**

NAOMBA kuuliza mamlaka husika, hivi usafiri wa mwendokasi ni huduma au mateso?

Nimeanza kwa kuuliza hivyo kwa sababu usafiri huu umegeuka mwiba mchungu kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Je, ni serikali imeshindwa kuendesha mradi huu au nini kinaendelea? Mara kadhaa tumeshuhudia viongozi wa serikali wakitoa matamko bila mafanikio yoyote.

Wiki iliyopita abiria wa usafiri huo, walijirekodi katika picha mjongeo iliyosambaa mitandaoni wakiwa wanaimba kuwa wamechoka manyanyaso ya mwendokasi.

Binafsi naungana nao kwa sababu tumechoka manyanyaso. Kama serikali imeshindwa mradi huu, wafunge na turudishiwe usafiri wa daladala kuliko haya mateso ya mwendokasi.

**Anna Peter,**
**Mbezi, Dar es Salaam.**

## Wizara ifuatilie mienendo ya walimu

**Mhariri,**

KUNA msemo unaosema ualimu ni mwito ikiwa na maana siyo kila mtu anaweza kuwa mwalimu.

Ualimu ni zaidi ya kufundisha masomo darasani, mwalimu ni mlezi anayelea tabia na maadili ya wanafunzi.

Hivi sasa kumeibuka tabia za ajabu kwa baadhi ya walimu ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.

Mbali na hilo, walimu wamekuwa wakifanya vitendo vya kikatili kwa wanafunzi kwa kutoa adhabu ambazo hazikubaliki.

Mfano unakuta mwalimu anamwadhibu mwanafunzi kwa kumchapa na fimbo hadi kichwani na wengine wanadiriki hata kuwapiga ngumi.

Wizara ya elimu kupitia maofisa wake wafuatilie mienendo ya walimu wao na kuwapa miongozo na maadili ya kazi.

**Selemani Said,**
**Mpanda, Katavi.**

## Viongozi wa dini wasipendelee vyama

**Mhariri,**

VIONGOZI wa dini ni kioo cha jamii na kimbilio la kuhifadhi na kuilinda imani, hivyo hawapaswi kuegemea chama chochote cha siasa, iwe chama tawala na hata vyama vya upinzani.

Nadhani wanasiasa wamemsikia Askofu Wolfgang Pisa aliyoyasema kuhusu mwongozo wa viongozi wa dini hasa wale wa Kanisa Katoliki, kuwa kutumika na chama chochote cha siasa ni kinyume na maadili na miongozo ya kiroho.

Kiongozi huyo aliwakumbusha watawa, mapadre, maaskofu na viongozi wengine wa kiroho wa Kanisa Katoliki, kuwa ni marufuku kuvaa fulana, kushika vipeperushi au kuhudhuria mikutano ya kisiasa.

Naungana na Askofu Pisa, kuwa haipendezi kwa viongozi wa dini kuwa na upande kwa maslahi yao binafsi.

**Vera John,**
**Old Moshi, Kilimanjaro.**



Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# Kauli ya Doyo kuhusu pamba isipuuzwe



KAULI ya mgombea urais kupitia Chama cha NLD, Doyo Hassan Doyo (pichani), kuhusu kuvunja Bodi ya Pamba Tanzania na kuweka mfumo wa soko huria shirikishi aliyoitoa Simiyu wakati wa kampeni wiki iliyopita, inagusa moja kwa moja kiini cha matatizo ya wakulima kote nchini.

Sekta ya kilimo, ambayo inachangia zaidi ya asilimia 25 ya Pato la Taifa (GDP) na kuajiri takribani asilimia 65 ya Watanzania (NBS, 2023), imekuwa ikikumbwa na changamoto za masoko yasiyo na ushindani na mfumo unaoelezwa kuwa kandamizi wa stakabadhi ghalani.

Tanzania inaelezwa kuzalisha wastani wa tani 250,000 – 300,000 kwa mwaka (TCB, 2022). Simiyu peke yake, maarufu kwa jina la “nyumbani kwa pamba,” huchangia zaidi ya asilimia 30 ya pamba yote ya Tanzania.

Licha ya mchango huu mkubwa, wakulima wengi wa Simiyu, Mwanza na Shinyanga wamekuwa wakilalamikia bei ndogo zinazotokana na mfumo wa ununuzi unaoathiriwa na wachezaji wachache wenye nguvu kubwa sokoni.

Mwaka 2021/22, mfano, bei ya pamba ilishuka hadi shilingi 1,050 kwa kilo, tofauti na matarajio ya wakulima waliokuwa wamewekeza gharama kubwa za pembejeo na kazi za mashambani.

Hali hii ndiyo iliyomfanya Doyo au Rais Mtoto kama anavyopenda kujiita, kueleza kuwa Bodi ya Pamba, badala ya kulinda maslahi ya mkulima, imegeuka kichocheo cha walanguzi.

Amesema kwamba mifumo ya kitaasisi isiyokuwa na uwajibikaji mara nyingi huzaa unyonyaji.

Uamuzi wake wa kuahidi kuondoa mfumo wa stakabadhi ghalani, ambao unalazimisha wakulima kuuza mazao kupitia ghala, badala ya soko huria, unaweza kuongeza uwazi na ushindani sokoni.

Huko Kenya, mageuzi ya sekta ya kahawa yaliyowawezesha wakulima kuuza moja kwa moja kwa wanunuzi wa kimataifa yameongeza kipato chao kwa wastani wa asilimia 20 zaidi (World Bank, 2021).

Zaidi ya pamba, Doyo anapendekeza kuondoa mfumo wa serikali kununua kwa lazima mazao kama mbaazi na dengu.

Kwangu hii ni hoja yenye mashiko kwa sababu mazao haya yamekuwa na soko kubwa India na Pakistan, lakini mara nyingi wakulima huuziwa bei ya chini kutokana na urasimu.

Takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ilisafirisha nje zaidi ya tani 80,000 za mbaazi mwaka 2020, zikiwa na thamani ya takribani dola za Marekani milioni 45 (BoT, 2021).

Ninaamini kuwa endapo wakulima wangepata uhuru wa moja kwa moja kwenye masoko, kipato kingekuwa kikubwa zaidi.

Kwa mantiki hiyo, sera za NLD zinazojengwa juu ya “uzalendo, haki na maendeleo” zinaonekana kulenga kumkomboa mkulima na kuhakikisha jasho lake linamletea tija.

Ikiwa mageuzi haya yangetekelezwa, taifa lingepata faida maradufu; kwanza, kuongeza kipato cha wananchi vijijini na kupunguza umaskini; pili, kuongeza mapato ya kigeni kupitia mauzo ya mazao kwa ushindani wa kimataifa.

Kwa ujumla, Doyo ameona mbali. Mageuzi anayoyapendekeza yanaendana na dhana ya kilimo biashara, badala ya kilimo cha kujikimu.

Hatua hii, ikitekelezwa kwa vitendo, inaweza kuwa nyenzo ya kuibadilisha Tanzania kuwa taifa lenye wakulima huru, wenye kipato cha uhakika, na hivyo kuchangia moja kwa moja katika kufanikisha ajenda ya maendeleo ya kitaifa.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

## Kimataifa

# Makamu wa Rais afikishwa kortini

KESI ya uhaini inayomkabili aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Sudan Kusini, Riek Machar ilifunguliwa Jumatatu iliyopita.

Ulinzi mkali uliimarishwa kwenye mitaa yote ya Jiji la Juba, ambalo ni makao makuu ya nchi hiyo.

Katika chumba cha mahakama maalum wakili wa Machar, alihoji kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Kuzuiliwa kwa Machar chini ya kifungo cha nyumbani tangu Machi, mwaka huu, kumezusha hofu ya kuzuka upya kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoharibu uchumi wa nchi hiyo changa Afrika.

Vita hivyo vilivyodumu kwa miaka mitano; 2013-2018 vina kiini cha makabila kufarakana. Makabila hayo ni Nuer na wapiganaji wa Dinka wanaomtii mpinzani wake wa muda mrefu, Rais Salva Kiir.

Chama cha Machar cha SPLM-IO kinakataa mashtaka dhidi yake na wengine 20 ambayo ni pamoja na mauaji, uhaini na uhalifu dhidi ya ubinadamu kwa madai ya kuhusika katika uvamizi wa wanamgambo wa Jeshi la White wanaotawaliwa na Nuer kaskazini mashariki mwa nchi hiyo.

Katika mahakama maalum, Machar alionekana hadharani kwa mara ya kwanza tangu kuzuiliwa kwake nyumbani Machi 2025.

Rais Kiir alimsimamisha kazi kwa amri mapema mwezi huo huku mashtaka yakifichuliwa.

Shirika la utangazaji la serikali ndilo liliruhusiwa pekee kufanya matangazo ya mahakama hiyo.

Geri Raimondo Legge, wakili wa Machar, alisema kuwa mahakama hiyo "ilikuwa kinyume cha sheria na batili" kwa sababu, alisema, Machar alikuwa na kinga kwa kuwa makamu wa rais aliyekuwa madarakani.

Washirika saba wa Machar walishtakiwa pamoja naye mapema mwezi huu, akiwemo waziri wa nishati.



*Makamu wa Rais wa Sudan Kusini, Riek Machar*

"Tunaomba mahakama iamuru kuachiliwa mara moja kwa Dkt Riek Machar Teny, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini, na washtakiwa saba kwa kukamatwa na kuzuiliwa kinyume na katiba," Legge aliiambia mahakama.

Mwendesha Mashtaka Ajo Ony'Ohisa Igele alizitaja hoja za upande wa utetezi kuwa "hazina msingi wowote wa kisheria na kwamba ni dhaifu."

Serikali inamtuhumu Machar kwa kuunga mkono Jeshi la White, wanamgambo wa kabila ambalo kwa kiasi kikubwa lina vijana wa Nuer, wakati wa mapigano na jeshi katika mji wa kaskazini mashariki mwa Nasir mwezi Machi.

Raia kadhaa waliuawa na zaidi ya watu 80,000 kukimbia makazi yao.

Kiir na Machar, wote wakiwa na umri wa miaka 70, walihudumu katika serikali ya umoja iliyokuwa dhaifu kama sehemu ya makubaliano ya amani ambayo yalimaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kiongozi wa zamani wa waasi, Machar amekuwa na uhusiano mbaya na Rais Kiir kwa zaidi ya miongo mitatu sasa.

***Makala haya yameandikwa kwa mara ya kwanza na TRT.***

# Habari katika Picha



*Mwenyekiti wa Joha Trust ambayo inayomiliki  Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Barbro Johansson, Profesa Anna Tibaijuka (katikati), akionyesha ujenzi wa Jengo la Tehama ambalo litawekwa vifaa vya kisasa vya kufundishia wanafunzi masomo ya sayansi ya akili mnemba 'Artificial Intelligence' (AI), Dar es Salaam juzi.*



*Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jacobs Mwambegele akiangalia mabengi kwa ajili ya mafunzo kwa watendaji wa vituo wakati wa uchaguzi baada ya kutembelea ghala la vifaa hivyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dodoma hivi karibuni. (Picha kwa hisani ya INEC)*



*Wanawake wakipanda maharage katika mashamba yao kufuatia msimu wa vuli kuanza kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa kama walivyokutwa katika Kata ya Kamachumu Wilaya ya Muleba, Kagera hivi karibuni. (Na Mpigapicha Wetu)*




*Baadhi ya wahitimu wa Kidato cha Nne wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Barbro Johansson wakiwa na vyeti vyao baada ya kukabidhiwa wakati wa Mahafali yao na maadhimisho ya miaka 25 ya shule hiyo, Dar es Salaam juzi.*

## Uhusiano

Na Anti MSHAURI





# Kuomba msamaha kunaponya maumivu

KARIBU msomaji wetu wa safu ya uhusiano ili uweze kujiongezea maarifa kutokana na mada mbalimbali tunazozijadili kila wiki.

Leo nitazungumza faida za kuomba msamaha kwa mtu uliyemkosea.

Hakuna mtu anayeweza kuepuka kufanya makosa katika maisha.

Kuna nyakati ambapo unaweza kumwumiza mtu na kumwomba msamaha ni moja ya mambo ambayo yanasaidia kupoza maumivu yake.

Kuomba msamaha pia hurejesha uhusiano ambao umevurugwa na kosa ulilolifanya.

Kuomba msamaha ni kitendo cha unyenyekevu kinacholeta amani, kurejesha upendo na kuleta mafanikio katika maisha ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

Kuomba msamaha kuna faida nyingi ikiwemo kusaidia kurejesha upendo na maelewano katika mahusiano, huondoa chuki na uhasama kati ya mtenda na mtendewa hivyo kuzuia ugomvi na mafarakano yasiyo ya lazima.

Pia msamaha hurejesha heshima na utu lakini pia kuweka amani ya moyo kwa aliyeomba msamaha.

Unaweza kuomba msamaha kwa njia nyingi kama vile kuzungumza na mlengwa uliyemkosea, kumpelekea zawadi kama maua na nyingine badala ya kuzungumza na njia nyingine ni ya kumwandikia ujumbe mzuri wenye maneno ya kuvutia ili kujutia ulichofanya.

Unapotaka kuomba msamaha hutakiwi kukurupuka bali kufanya maandalizi yako binafsi na kuangalia uliyemkosea yupo katika hali gani.

Kama uliyemkosea ni mume, mke au mpenzi wako chagua muda tulivu ambao mtu wako yupo tayari kukusikiliza.

Epuka kuomba msamaha ikiwa hampo kwenye mazingira magumu au vurugu.

Unapomwomba msamaha mpenzi wako, tumia lugha rahisi na yenye kugusa moyo.

Ni lazima kuonyesha kuwa unalilolisema linatoka moyoni na unalisema kwa dhati.

Epuka kuongea kwa ujeuri au kulazimisha.

Msamaha wa kweli hutoka moyoni na kwa ndugu, jamaa au rafiki jitahidi muwe katika mazingira rafiki ya kutekeleza hilo.

***Tukutane wiki ijayo.***

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***



# Fahamu vazi rasmi la Burkina Faso

WAKATI Tanzania ikiwa inasuasua kupata vazi la taifa, Burkina Faso tayari imetangaza vazi lake la taifa.

Rais wa Burkina Faso, Ibrahim Traore, alitangaza uamuzi huo hivi karibuni huku akipiga marufuku watumishi wa umma kuvaa suti katika shughuli mahsusi za kiserikali.

"Sahau kuhusu suti, Burkina Faso inabadilisha namna watu wanavyovaa kazini," ilisomeka sehemu ya taarifa kwenye ripoti ya kimataifa iliyochapishwa Septemba 2025.

Taarifa hiyo ilielezea jinsi taifa hilo linavyopigia debe mavazi ya ndani ya Bara la Afrika kama njia ya kukuza utamaduni na utambulisho.

Ofisi za serikali na mashirika binafsi nchini humo, wanaume wengi wanajivunia kuvaa mavazi ya kienyeji kama vile faso dan fani, kitambaa cha pamba kilichofumwa kwa mikono ambayo ni nembo ya taifa hilo.

# Tumia manjano, sukari kuzibua matundu usoni


MATUNDU ya usoni yanapoziba yanasababisha uchafu kuganda na uso kushindwa kuwa sawa.


Hilo linaweza kusababisha uso wako kuwa na chunusi kwani ngozi inashindwa kupumua vizuri.

Ukiona hivyo, tumia manjano na sukari kufanya scrub usoni.

Chukua manjano iliyosagwa, changanya na sukari kisha weka rose water kiasi kisha pakaa usoni kwa kuscrub.

Fanya hivyo mara kwa mara kwa matokeo mazuri zaidi.







# Kizz Daniel katika tuhuma nzito

Na Mwandishi WETU

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, Kizz Daniel, ametuhumiwa kutapeli waandaaji wa matamasha na kusababisha hasara kubwa.

Kampuni ya Bankiis imeibua tuhuma hizo huku ikiwatahadharisha waandaaji wa matamasha wasimchukue kutokana na tabia yake hiyo.

Kupitia ukurasa wao wa Instagram, Bankiis wameweka wazi kuwa Daniel amekuwa akiacha mapromota katika wakati mgumu na kukatisha tamaa mashabiki.

"Waandaaji wa matamasha wanaonywa vikali dhidi ya kum-book Kizz Daniel. Kutokana na uzoefu uliopita, ameonyesha tabia ya kutojitokeza kwenye show…"

"Zaidi ya hapo, kwa sasa hana mashabiki wa kutosha au nguvu ya kibiashara ya kuleta faida wanazotarajia mpromota. Yeyote anayefikiria kufanya naye kazi anatakiwa kufikiria kwa makini, kwani nafasi ya kupata faida ni ndogo sana ikilinganishwa na hatari kubwa iliyopo," ilisema taarifa hiyo ya Bankiis.

# K-Lynn alia na watoto yatima kudhulumiwa

Na Mwandishi WETU

MISS Tanzania 2000, Jacqueline Ntuyabaliwe Mengi, almaarufu K-Lynn, amemwandikia barua ya wazi Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu changamoto zinazowakumba watoto yatima.

Katika barua yake hiyo aliyoiweka kwenye ukurasa wake wa Instagram, K-Lynn amesema mara nyingi haki za watoto kupata malezi na urithi hazitekelezwi.

Amesisitiza kuwa dhuluma hiyo inawaathiri zaidi watoto wanaopoteza baba, ambao wanakosa usalama na ulinzi wakati wanapohitaji uthabiti.

Kutokana na hilo, anamwomba Rais Samia kwamba wasimamizi wa mali za marehemu wawajibishwe na kuwepo na ukaguzi mkali dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka.

"Mama waliyoachwa wakiwa bado vijana na watoto wao wapate ulinzi maalumu ili wasibaki bila msaada kutokana na mianya ya mifumo ya udhaifu…"

"Viongozi wa serikali wawe mstari wa mbele kulinda haki za watoto na kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayepitia dhuluma mara mbili; kupoteza mzazi na kutopewa haki ya maisha ya baadaye," ameandika K-Lynn.



# Kane avunja rekodi ya Ronaldo, Erling



**Munich, Ujerumani**

MSHAMBULIAJI wa FC Bayern Munich; ambaye ni mfalme wa mabao kutoka Uingereza, Harry Kane sasa ameipiku rekodi ya Cristiano Ronaldo wa Al Nassr pamoja Erling Haaland wa Manchester City kwa kufunga magoli 100 katika mechi 104.

Kane anakuwa mchezaji wa kwanza duniani kufikisha magoli 100 katika mechi 104, ambapo awali Ronaldo pamoja na Haaland walitumia mechi 105 kufikisha idadi hiyo ya magoli. Ikumbukwe Ronaldo aliishikiria rekodi hiyo kwa miaka 14.

Nyota huyo juzi alifunga magoli mawili kwenye mchezo wao dhidi ya SV Werder Bremen, ambapo FC Bayern Munich waliigaragaza timu hiyo 4-0, magoli yakifungwa na Kane magoli 2, Konrad Laimer goli 1, pamoja na Jonathan Tah goli 1.

Kane kwenye tuzo za Ballon D'or zilizofanyika hivi karibuni nchini Ufaransa, alishika nafasi ya 13 katika orodha ya wachezaji 30 bora duniani.

Mpaka sasa Harry Kane amefunga jumla ya magoli 15 na kutoa pasi za mwisho za magoli matatu katika michezo nane waliocheza FC Bayern Munich.

Wakati huohuo, Cristiano Ronaldo naye anaendelea kuweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyefunga magoli mengi zaidi duniani akiwa na mabao 946.

Ronaldo mara kadhaa akihojiwa amesikika akisema ana malengo ya kufikisha idadi ya magoli 1000 katika michezo yote kuanzia ngazi ya klabu hadi timu ya taifa kabla hajastaafu.



# Yanga, Simba zapenya kibabe

Na Mwandishi WETU

MABINGWA wa soka Tanzania, Yanga wamejihakikishia kuingia raundi nyingine ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya juzi - Jumamosi kuibuka kidedea kwa ushindi wa mabao 2-0, dhidi ya Timu ya Wiliete ya Angola.

Magoli ya Yanga yalifungwa na Pacome Zouzoua katika dakika ya 71, huku bao la kulinda ushindi huo likiwekwa kimiani na Aziz Andabwile dakika ya 87.

Katika mchezo wa juzi, Yanga walianza kwa kusuasua, kana kwamba wanawasoma wapinzani wao, kwani walishindwa kupata bao hata moja katika kipindi cha kwanza, licha washambuliaji wake kupata nafasi za wazi kufunga, lakini walishindwa.

Yanga, ambayo imesajili wachezaji wenye kasi na mbinu lukuki uwanjani, kipindi cha pili, kiliwafanya “kukaza msuli” ndipo walipofanikiwa kupata mabao hayo mawili na kuwa washindi.

Kutokana na ushindi huo, Yanga SC wamefanikiwa kusonga mbele kwa jumla ya mabao 5-0, baada ya kushinda mchezo wa kwanza kwa mabao 3-0 wakiwa ugenini jijini Luanda, Angola wiki iliyopita.

Wakati huohuo, timu nyingine ya Tanzania, Simba, nayo jana ilisonga mbele kwenye michuano ya mabingwa Afrika baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Timu ya Gaborone United ya Botswana.

Kutokana na matokeo hayo, Simba inasonga mbele kuingia raundi nyingine kwa kuwa na jumla ya mabao 2-1 didi ya timu hiyo.




*Kiungo mkabaji wa Yanga SC, Azizi Andambwile akishangilia moja ya bao alilofunga katika mchezo wao dhdi ya Wiliete*

Katika mchezo wao wa kwanza, Simba – ikiwa ugenini nchini Botswana, ilifanikiwa kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Gaborone United, wiki mbili zilizopita.

Timu hizo mbili za Tanzania, zimeanza vyema na sasa hamu ya mashabiki ni kuona zinafanya vyema kwenye michezo inayofuata.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION